# *Nimtendeje Yesu Aitwaye Kristo?*

Bwana akubariki, Ndugu Vayle. Habari za asubuhi, marafiki. [Kusanyiko linasema, "Njema, Ndugu Branham."] Mimi sikuzote ninachelewa. Billy alikuwa ananiambia nimechelewa, asubuhi hii, nami nina kama mahojiano thelathini hivi ya faragha, na nimefanya mawili, kwa hiyo, naamini mawili ama matatu. Kwa hiyo siwezi tu kumfikia kila mtu, mnajua, na huku watu wanangojea, nao wamekuwa wakingojea kwenye orodha kwa miezi na miezi. Naye Bwana amekuwa akifanya mambo makuu humo. Loo, Ye—Yeye ni Mungu wetu. Sivyo? ["Amina."]

2 Sasa nina hakika, asubuhi hii, ya kwamba sote tuna habari za msiba mkuu uliotukia kwa taifa hili, wa kupotelewa na Rais wetu, Bw. Kennedy. Ingawa sikukubaliana na mtu huyo katika siasa zake na katika dini yake, lakini hata hivyo yeye hastahili kufa namna hiyo. La. Na kuwaacha hao watoto wadogo nyuma, huku hawana baba. Na mama ambaye ni. . .Bibi. Kennedy, ingawa kweli nisingekubaliana naye, na mwenendo wake na kadhalika, labda, lakini, kumbukeni, yeye ni mama. Hivi karibuni amepoteza watoto wake wachanga, kisha akampoteza mumewe. Naye aliangukia papo hapo pajani mwake, na damu ya mume wake ilimwagikia pajani mwake. Hilo ni jambo baya sana.

3 Hivi umewahi kuwazia. . .Wakati mwingine tunafikiria ya kwamba yeye ndiye anayeanzisha mitindo nchini, katika staili na kadhalika. Hilo laweza kuwa ni kweli, pia. Lakini je! mlijua, Bibi. Kennedy kamwe hajapata kusikia mmoja wa Jumbe hizi ninazohubiri juu ya jambo hilo. Kama angesikia moja ya Jumbe hizo, huenda akatenda vinginevyo. Na baadhi ya dada zetu wanaousikia, na hata hivyo hawatautii. Unaona? Unaona? Unaona? Yeye alilelewa Mkatoliki; hayo ndiyo tu ajuayo. Sina neno juu ya jambo hilo, unaona. Yeye . . . Huo ni utaratibu fulani. Sina neno dhidi ya hao watu, Wakatoliki. Huo ni utaratibu, utaratibu wa Kikatoliki, kama vile tu Presbiteri, Methodisti, ama yo yote yale, unaona, ama Pentekoste, yo yote yale. Ni huo utaratibu, si hao watu.

4 Bw. Kennedy, nafikiri, alifanya ka—kazi nzuri kwa kuwa Rais. Nao moyo wangu unamwonea huruma mkewe. Nami ninasikia huzuni kweli juu ya jambo hilo, ya kwamba hata taifa letu lenyewe lingefanya, majambazi na kadhalika katika taifa letu, wangefanya jambo kama hilo.

5 Iwapo wewe huwezi kukubaliana na mtu, sawa, na kuchukua msimamo wako; na hakuna sababu ya kumuua mtu mwingine, kwa sababu tu ya mambo kama hayo. Na hao watoto wadogo wanajua, kasema, jamaa mmoja mdogo alisema, "Sasa sina mtu wa kucheza naye tena. Baba ameaga dunia." Unaona?

Kwa hiyo daima nimewaza hiyo ingekuwa hali yangu, siku moja. Karibu jambo hilo limetukia mara nyingi, kama mjuavyo, juu ya kupigwa risasi katika mataifa ya kigeni; wakati imewalazimu kushikamanisha miili yao juu yangu, kunifanya nisipigwe risasi, kutoka mbali.

6 Kwa hiyo kama mtu akifa namna hiyo . . . Lakini, hiyo ndiyo—ndiyo gharama inayolipwa, inayoambatana na fahari ya mambo mbalimbali. Mnaona? Nafikiri tuna wastani wa kila Rais wa nne, mmoja kati ya wanne, anauawa, nami naona vibaya sana juu ya jambo hilo. Ni aibu kwamba tungekuwa na mtu kama huyo Marekani, angefanya jambo kama hilo.

7 Na sasa, hata hivyo, kama nilivyosema, si—sikukubaliana na siasa zake. Mimi ni . . . sikubaliani, sikukubaliana na mawazo yake ya yale aliyokuwa akijaribu kufanya. Lakini, mnaona, yeye ni mtu mwingine. Wala sikukubaliana na utaratibu wake wa dini. Kweli si—sikukubaliana na jambo hilo. Lakini, hata hivyo, yeye—yeye alilelewa namna hiyo. Hivyo—hivyo ndivyo ilivyokuwa. Kama nilivyosema, labda angalisikia jambo fulani tofauti, ingalikuwa vinginevyo.

8 Tuna ja—jambo hapa tufanyalo, kwamba kila mmoja wa watu wetu anapokufa, ama cho chote kile, hata ingawa kutoka . . . Nafikiri kama—kama kanisa la Kimarekani, kama kundi la Wamarekani . . .

Wamarekani walimpigia kura Bw. Kennedy awe Rais. Na hilo lilikuwa . . . Hiyo ndiyo sababu sisi ni demokrasia. Mimi sikumpigia kura Bw. Kennedy. Nilimpigia kura Bw. Nixon, maana nilimjua Bw. Nixon, kibinafsi. Nami ni—nilimpenda, ndipo nikampigia kura, mimi mwenyewe, kwa kuwa nilimpenda. Lakini watu wa nchi hii, Wamarekani, raia wenzangu wa nchi hii, walimchagua Bw. Kennedy. Na jinsi walivyofanya jambo hilo, vema, hiyo ni kati yao na Mungu, lakini jambo ndilo hilo.

9 Bali nafikiri, kwa ajili ya mama huyu, mwanadamu, mama wa watoto, Bibi Kennedy, tungeweza kusimama tu kwa muda mdogo wa maombi kwa ajili yake?

10 Bwana Yesu, sisi binadamu, tunahurumiana sisi kwa sisi. Nasi tunasikitika, Bwana, ya kwamba Rais wetu alipigwa risasi jinsi alivyopigwa, katika mauaji ya kinyama. Nasi tunasikitika sana kwamba taifa letu limefikia kiwango hiki, ya kwamba watu kama hao wako—wako katika taifa letu, ambao wangemuua mwanadamu kinyama; kama walivyomuua yule ndugu mweusi si muda mrefu uliopita, nao wakampiga risasi tu kinyama kabisa, kwa ubaguzi wa rangi. Nasi tunasikitika sana kwamba watu

kama hao wanaishi miongoni mwetu, Bwana. Sisi, unyonge wetu, umesababisha haya.

11 Nasi tunamwombea Bibi Kennedy, huyo mke wa huyu, Rais. Na tunajua hao watoto wadogo wanamtafuta baba ya— yao, aliyewaacha siku chache kabla ya hapo, mtu mwenye furaha, naye akatambaa na kucheza nao sakafuni. Sasa wao hawana baba. Na kwa ajili ya mwanamke huyo ambaye... mkewe, ambaye mumewe alianguka kwenye paja lake, na damu yake ikamwagika kwenye gauni lake; hivi karibuni tu alimzika mtoto wake mchanga.

12 Na hata hivyo, Bwana, twaweza tuamini mwanamke huyo kuwa makosani, kwa vile—vile—vile ameanzisha mitindo katika taifa, kuhusu anavyovalia na kadhalika; lakini hilo— hilo lingeweza kuwa kwa Wamarekani, kwa jumla, wao, kwamba hivyo ndivyo wanavyotaka. Kwa hiyo sisi—sisi tunamwombea, asubuhi ya leo, ya kwamba utamsaidia. Basi naomba kuwe na wakati katika msiba huu mkubwa ambapo atampata aliye Kweli, Yesu Kristo! Jalia jambo hilo, Bwana, Wewe ambaye Ndiye tu unayeweza kutoa amani na faraja katika wakati wa shida.

13 Basi tusaidie, Bwana, kuendelea kuwa, kwa mioyo yetu yote, nuru inayong'aa, kwamba hatujui ni wakati gani ama ushawishi gani tunaoweza kuwa nao juu ya mtu mwingine. Basi jalia tuangaze Nuru ya Kristo hata atakapokuja. Ndipo yule Mchungaji Mkuu wa kundi, Ambaye anajua haki yote, ataijazi kila dhambi, Naye atajua tu jinsi ya kufanya jambo hilo. Basi hadi wakati huo, tunajiweka mikononi Mwako, kwa ajili ya upendo Wako na huruma juu yetu. Katika Jina Lake Yesu. Amina.

14 Naam, sidhani kuna mtu anayestahili kufa namna hiyo. Naam, Bw. Lincoln hakustahili kufa namna hiyo. Bw. McKinley hakustahili kufa namna hiyo. Huey Long hakustahili kufa namna hiyo; hata mmoja wa jamaa hao. Mimi siamini katika jambo hilo. Mauaji, hilo ni jambo baya. Vijana wetu hawakupigana katika nchi za ng'ambo kwa ajili ya jambo kama hilo. Bendera yetu haikupandishwa kwa ajili ya kitu kama hicho. Sisi si raia wa Marekani kwa jambo kama hilo. La. Ingawa, taifa letu limepotoshwa na kugaagaa kwenye dhambi, ndiyo ambayo—ndiyo ambayo inayofanya mambo haya. Hiyo ni dhambi.

15 Naam, leo tuna-...Nitafundisha shule ya Jumapili, na mambo kadha ambayo ningetaka kuliambia kanisa. Na hiyo ni, jambo la kwanza, ningetaka mnisamehe kwa kuwacheleweshe sana Jumapili asubuhi ninapokuwa na Jumbe hizi. Halafu kama Bwana ata-...Sababu ya kufanya jambo hili, ni kwa sababu kwamba mi—mimi niko hapa miongoni mwa watu wangu na ni—ninafundisha mafundisho kwa nguvu niwezavyo. Sifundishi mafundisho haya huko nje mahali pengine. Mimi husimama tu katika—katika kanuni muhimu tu za Injili. Lakini mafundisho

haya ambayo ni magumu, ni—siyafundishi huko nje ma—mahali pengine. Ndipo basi, hapa, inanichukua saa moja, wakati mwingine, masaa mawili ama matatu, kumaliza Ujumbe wangu. Nami ninawaweka hapa wakati mwingine, saa sita u nusu, saa saba. Na hilo ni jambo dogo tu ukilinganisha na yale niliyokuwa ninafanya. Ningekaa usiku kucha, karibu usiku kucha, wakati mwingine. Nimeenda, tumeanza, wakati mwingi, saa mbili na kuondoka kwenda nyumbani usiku huo saa nane ama saa tisa, hiyo ni kweli, kutoka kwenye mikutano yangu.

16 Lakini ni—ni—nitajaribu, nitakapokuja pamoja nanyi tena, na kidogo tu—kidogo . . . ibada ya mahubiri badala ya kufundisha sana jambo hili, isipokuwa niwaambie hapo kabla ya kwamba itakuwa ni jambo fulani. Maana, nina zile Baragumu Saba, ninaamini, zinazokuja, ambazo zinafungamana moja kwa moja kwenye ile Muhuri ya Sita. Wakati ile Muhuri ya Sita ilipolia, Baragumu zote Saba zililia wakati mmoja, mnaona. Na kwa hiyo sisi . . . Ningetaka kulipa Kanisa hizo kabla ya Kuja Kwake, kama . . . ama kuondoka kwangu, ama cho chote kile, nikiweza.

17 Sasa, kama tukifanya jambo hilo, basi tutawajulisha kabla ya wakati. Na labda basi, kama tunavyoona asubuhi ya leo, kumbi zina msongamano wa watu, na kwenye kuta, na kila mahali, tutajaribu . . . Tuna mahali sasa huenda tukaweza kupapata hapa. Panakaa kama watu elfu tatu, na ni jumba zuri la mikutano la shule fulani iliyopo papa hapa juu yetu hapa. Basi zile Baragumu Saba, tutajaribu kuzihubiri kule shuleni. Basi huo utatoa nafasi kubwa sana ya kuketi, mnaona, ili kwamba tuweze kuwaingiza watu.

18 Tunataka kutangaza, huko New York, hivi karibuni tulikuwa na wakati mzuri sana. Jumba la Mikutano la Morris pale, ilitulazimu kuwarudisha watu, kila usiku. Walikuwa wamesongamana mle ndani. Moto . . . Tajiri wa mahali pale . . . Mkuu wa zimamoto angepafunga mahali hapo kama tungewaruhusu kusimama, wamesongamana namna hiyo. Na basi ilitubidi kuwarudisha. Nao watu huko barabarani, wakitembea huku na huko barabarani, wakiomba kwamba mtu fulani angechoka na kusimama atoke nje, ili kwamba waweze kuingia na kupata kiti. Mnaona? Mtu mmoja tu, wao wanangojea tu kule nje kwa ajili ya mtu huyo mmoja, wapate kuingia. Naye anayefuatia mlangoni, halafu wao wanamruhusu mmoja aingie namna hiyo. Mtu mmoja anapoamka na kutoka nje, ilimbidi kwenda nyumbani mapema, vema, wao wangeingia na kushiriki kiasi hicho cha jambo hilo. Mnaona, wangekuja. Ni kundi zuri sana, sana la watu. Nami ninaamini ulimwengu, kanisa la Kikristo, lina njaa ya Mungu.

19 Sasa mi—mi—mimi ninaamini ya kwamba . . . Asante, ndugu. Ni—ninaamini ya kwamba—ya kwamba Mungu atatujalia nafasi hii, ambapo tunaweza kukutanika pamoja na kuwa na hizo

Baragumu Saba za mwisho. Mimi ninapenda niongozwe kufanya mambo hayo, ili kwamba mpate kujua.

20 Halafu kwenye kifunguakinywa cha wafanya biashara... Kwa kawaida, mkutano wao pale, nafikiri wao walisema walikuwa na kati ya hamsini hadi mia kwenye kifunguakinywa chao. Na asubuhi hiyo wao waliuza tikiti elfu moja na mia saba, na wakakodisha mahali paliposalia, wapate kupajaza mahali hapo. Na kila ujia, na kila mahali kwenye kuta, na huku na huko kwenye vipandio, kulikuwa kumesimama watu. Na wahudumu wenye vyeo vya juu, baadhi ya makasisi, na—na kadhalika, walikuwapo pale kuusikia Ujumbe. Na kwa hiyo, nasikia, naamini hilo lilisaidia kidogo. Huenda ungefanya za—zaidi, vizuri zaidi kuliko vile tungefikiria kweli ingekuwa.

21 Naam, basi, usiku...Tutakuwa na...Ujumbe usiku huu, Bwana akipenda, juu ya—juu ya somo la—la jinsi, juu ya hali zako pamoja na Kristo. Na sasa huo uta-...Utakuwa mfupi. Tunataka kuanza, ninataka kuwa jukwaani saa moja u nusu. Kama...Mnaanza saa ngapi kwa kawaida, saa moja u nusu? [Ndugu fulani anasema, "Tunaanza saa moja u nusu, bali tutaanza saa moja."—Mh.] Loo, moja, nami nitakuwa jukwaani ifikapo saa moja u nusu, na hiyo yapaswa kuniondosha ifikapo saa mbili u nusu, Bwana akipenda, maana mimi—mimi tu... nitaharakisha tu niwezavyo, nitaanza kujizoeza.

22 Halafu jambo jingine, ni, ikawa huenda ikawa wageni fulani wanasikia watu wakicheka. Maana, ninajaribu kuondoka hapa, bali siwezi kufanya hivyo. Kwa namna fulani ni...natumaini halitasikika la kukufuru, bali mamangu alizoea kusema, watu wanapokutanika pamoja namna hiyo, ni kama machujo ya asali ya mtama katika asubuhi yenye baridi. Mwajua, ni nzito, na inachuruzika polepole. Na kwa hiyo hivyo ni karibu na kama vile ilivyo. Mimi huenda polepole katika Jumbe hizi, kwa kuwa u—utamu wa miwa ya Mungu, mwajua, kwa namna fulani hutuvuta pamoja. Nami si—si—si-, nisingetaka jambo hilo vinginevyo. Ni—ninalitaka tu namna hiyo. Ambapo, ninakumbuka tulizoea kusimama na kuimba wimbo ule.

> Kibarikiwe kifungo kitufungacho
> Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
> Ushirika wa watu wenye nia moja
> Ni kama ule wa huko Juu. Mnaona?
>
> Tunapoachana,
> Linatuumiza kindani;
> Lakini tungali tutakuwa tumeunganishwa moyoni,
> Na kutumaini kukutana tena.

23 Nami ni—ninatumaini kwamba jambo hilo daima litakuwa lengo le—letu hapa. Wengi wa hao watakatifu wa kale wamelala mauti tangu wakati huo, bali tungali tumeunganishwa moyoni.

Nami nafikiri ono lile asubuhi ile, kuwaona wao kule ng'ambo, na utukufu uliobarikiwa wa kimo cha ujana wa mwanamume na utu uke, wangali wanaonekana kama walivyokuwa hapa, walipokuwa hapa duniani. Nafikiri wanangojea kuja kwetu. Siku moja tutajiunga nao, Mungu akipenda. Sasa mimi—mimi . . .

24 Basi kumbukeni ibada, ibada za nyimbo zitaanza saa moja usiku wa leo, badala ya saa moja u nusu.

Halafu, juma lijalo, niko huko Shreveport, Louisiana, na kule kwenye Maskani ya Uzima Shreveport, Louisiana. Basi nafikiri wao wanajaribu kulipata hilo jumba la mikutano upande wa pili wa barabara. Ndugu Moore alinipigia simu jana usiku, kasema wao . . . Ni mkutano wa kila mwaka, nao wanatarajia wingi wa watu.

25 Ninataka kutoa ushuhuda mdogo kabla tu sijasoma Maandiko. Bi—bibi fulani alikuwa ameketi hapa juzijuzi, kulikuwa . . . Niwaambie ushawishi ulivyo wa mtu fulani akimwombea mwingine. Nilitazama tu kwa bahati nikamwona bibi mwingine ndiyo kwanza mimi . . . Margie Cox, mke wa Ndugu Rodney Cox anayeketi hapa. Na juma lililopita, ninaamini ilikuwa hivyo, tulipokuwapo hapa, Roho Mtakatifu alikuwa anatoa upambanuzi kila mahali jengoni, mwajua, jinsi watu walivyoambiwa. Naye alikuwa ameketi . . . Yeye ameketi papa hapa sasa. Lakini alikuwa kule nyuma mahali fulani. Na—nami nikatazama kule, na alikuweko bibi ambaye—ambaye aliitwa, aliyekuwa na ugonjwa wa kisukari. Naye Margie alikuwa . . . Na katika lile ono ilikuwa ni Margie. Naye Margie alikuwa amesimama pale; na hata hivyo nilitazama chini, nikamwona, na ilikuwa ni . . . Ndipo nikawaza . . . Nami nikatazama kumwona mwanamke huyu mwingine, naye Margie alikuwa katika lile ono, bali ile Nuru ilikuwa juu ya yule mwanamke. Kwa hiyo ni—nikaangalia.

26 Basi nikawaza, vema, kama nikimwita Margie, wao watasema, "Bila shaka, huyo, bila shaka." Mtu fulani anawajua, aseme. "Mbona, yeye—yeye . . . Mumewe ni mmoja tu wa marafiki wasiri wa—wake. Wao wanaishi pamoja, wanalala pamoja, wanawinda pamoja, na—na kila kitu. Bila shaka, hiyo ni, yeye angejua jambo hilo." Lakini Margie hakujua jambo hilo. Lakini nilimwita yule bibi mwingine, ambaye alikuwa . . . Ninaamini, alikuwa ni dada fulani aliyetoka Chicago, kama nilivyotambua baadaye.

27 Ndipo ikawa, ya kwamba kwenye nini hii yake. . . . kiwandani, wao wanafanya uchunguzi wa kisukari. Naye—naye alikuwa na kisukari. Na kwa hiyo alikuwa anaenda zake, juzi, kwenye zahanati kwa ajili ya hilo. Na—na kwa hiyo alipotaja jambo hilo, ndipo nikamkumbusha jambo hili. Ndipo nikasema, "Njoo hapa, Dada Margie." Nami nikamwambia jinsi

alivyokuwa anapata ganzi kwenye mikono yake, na—na jinsi ambavyo kule kujisikia vibaya sana.

Maskini bibi huyo anafanya kazi mchana na usiku, karibu mchana na usiku, kule juu, ku-. . .maskini mama mwaminifu, kumsaidia mumewe kulipia makazi yao wanayojaribu kujenga. Basi—basi yeye na dada yake mdogo, Nellie, na Charlie, huyo ni Ndugu ya Rodney, mkewe, na hao wote wakifanya kazi pamoja kwenye viwanda hivyo kule, wakijitahidi wawezavyo. Nao wakistahimili shutumu. Wanaachilia nywele zao zikue, na kutoa vipodozi, na vitu vya namna hiyo, walipokuwa Wakristo. Ninaamini katika kutoa sifa mahali panapostahili sifa. Nami bila shaka ninawapenda sana hao vijana wanawake wawili.

28 Basi nikamshika mkono na kumwombea. Ndipo akapanda akaenda, nao hawakuweza kupata kisukari cho chote mahali po pote. Kimeondoka, namna hiyo.

Bibi fulani aliketi papa hapa ndani mahali fulani, aliyeitwa, naye alikuwa ni dada fulani jina lake Bruce. Simwoni asubuhi ya leo, lakini yeye daima. . .Yeye ni mwanamke anayependa sana kuomba. Basi mwanamke huyu akaingia na, ilikuwa mara ya mwisho nilipokuwa hapa, na hakukuwako na ka—kadi za maombi za kusambaza, wala cho chote kile, kwa hiyo kusingekuweko na mtu ye yote, kusingekuweko na mstari wa maombi, kwa hiyo wao wakanini hii tu. . . Roho Mtakatifu akaita tu kwenye mkutano.

29 Na maskini huyu Bi Bruce, yeye ali—aliponywa mara moja, yeye mwenyewe, kansa. Naye—na daima alikuwa tu na mzigo moyoni mwake kwa ajili ya mtu mwingine, naye alikuwa anaomba tu. Basi kulikuwako na bibi fulani kutoka Louisville, aliyekuwa anakufa, kansa kwenye koo. Ndipo alipokuwa anaomba, Roho Mtakatifu, anaenda moja kwa moja hadi kwa mwanamke yule, anamwita, na kilo Roho alichofanya, kumwambia alikuwa ni nani, akamwambia, hasa, yeye alikuwa nani, na shida yake ilikuwa ni nini, na kuhusu yeye kuwa na kansa, kisha akasema, mambo yangekuwa sawa. Ndipo maskini bibi yule akaenda nyumbani.

Siku kadha baada ya jambo hilo, alianza tu kukabwa sana, karibu afe, koo lake likavimba mno. Akakohoa mara moja kwa nguvu sana, ndipo ile kansa ikaruka ikatoka. Naye yu mzima kabisa. Mnaona?

30 Kilichotukia, mnaona, kile kitumba, chenyewe, ni kitu kinacholeta mauti ambacho kina uhai ndani yake. Mnaona? *Kansa*, inayotokana na ne—neno, neno la madawa, la "kaa," ambayo ina maana kwamba ina miguu mingi sana, kama yule—yule kaa unayempata kutoka baharini na—na anakufyonza damu yako. Basi kivimbe hiki kinachosababisha mauti kilichokuwa kwenye koo lake, kilikuwa, hivyo ndivyo kilikuwa kinafanya.

Naam, mnaona, mimi sijishughulishi na kile kivimbe. Ninajishughulisha na uhai uliomo katika hicho kivimbe. Mnaona? Uhai ulio katika kile kivimbe ndio tunaoshughulikia. Mnaona? "Katika Jina Langu watatoa pepo." Neno *pepo* ni "mtesi," kama wa mwili. Basi huyu alikuwa ni ibilisi. Na ndipo uhai ulipotoka kwenye kile kivimbe, bila shaka, jambo hilo lilifanya kivimbe hicho kianze kuvimba.

31 Ni kama tu mbwa mdogo aliyekanyangwa barabarani, kitu kama hicho, hebu acha akae hapo kwenye jua kwa siku chache, halafu, naye anakuwa maradufu ya ukubwa wake.

Vema, hicho ndicho kilichokuwa kinamfanya maskini mwanamke yule kupata hali mbaya zaidi. Mara nyingi nimeelezea jambo hilo. Kama ukizidiwa, hiyo ndiyo ishara madhubuti kwamba umekwisha kuponywa, mnaona. Na kwa hiyo ilikuwa tu inazidi kuwa hali mbaya wakati wote, na kumziba pumzi, maana kilikuwa kinavimba. Nayo. . . Lakini ilikuwa imelegea, uhai ulikuwa umeitoka. Basi kukohoa kwake namna hiyo, mnaona, [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] namna *hiyo*, ikaruka, kukailegeza iachane na huo mwili mwingine. Na kitu hicho kilichokufa, mwili tu usio na uhai ndani yake, kansa imeondoka, iliruka nje, mnaona, ikaangukia nje.

32 Kwa hiyo, hilo ndilo, mwili ulitoka wakati huo. Hicho kilichotoka si ibilisi. Hiyo ilikuwa ni nyumba alimoishi. Alitoka kwa sababu imani ya huyo mwanamke katika yale aliyoambiwa, kujua Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hiyo ndiyo iliitoa hiyo kansa, hiyo ndiyo iliutoa ule uhai.

Sasa, yeye angalienda—angalirudi kwa daktari, naye daktari akasema, "Upuzi, ki—ki—kitu hicho kingalipo jinsi kilivyokuwa daima." Lakini hiyo ilikuwa kweli, kivimbe kilikuwapo, bali si ule uhai, haukuweko. Mnaona?

33 Naam, vipi kama hiyo ilikuwa mahali ambapo isingeweza ku—kutoka?

Hiyo ndiyo ile picha? [Ndugu Neville anamwambia Ndugu Branham, "Hiyo ndiyo picha ya kivimbe kilichotoka kwa Bibi Baker, kutoka kule Springville, Indiana. Naye. . . Hii ni picha iliyokuzwa, aliyotapika, baada ya maombi."—Mh.] Hii hapa ile picha ya kile kivimbe kutoka kwa Bibi Baker, kutoka Springfield, Indiana, iliyotoka, baada ya maombi. Hiyo ndiyo picha yake. Mnaona, huo ndio mwili ambamo ibilisi aliishi ndani yake.

Kama tu vile unavyoishi katika mwili huu unamoishi; huenda ukawa ni mdogo, mkubwa, wenye nywele nyekundu, wenye nywele nyeusi, wo wote ule. Mnaona? Ibilisi aidha anaishi katika mwili huu, ama Kristo huishi katika mwili huo. Vema, basi uhai unapotoka ndani yake, mwili wako ungali hapa duniani, mnaona, bali uhai haumo mle.

Wakati ule uhai ulipotoka, ule mwili ulikuwa ungali pale. Ndipo ukararuliwa kutoka kwenye mwili wake na ukatupwa nje, huo mwili ukatoka.

Lakini kama uko katika mahali usipoweza kutoka, basi moyo wako hauna budi kuchukua kitu hicho kilichokufa na kuisafisha damu, kila mara unapopiga. Jambo hilo linasababisha homa, na kila kitu kingine, kwa maana ni ambukizo. Mnaona? Na moyo wako hauna budi . . . Nafikiri moyo huisafisha damu wakati inapopita. Sivyo, Dada Dauch? Nafikiri hiyo ni kweli. Moyo, unapopiga, unasafisha. Nesi, mwajua, na mwingine anayeketi hapa mbele yake. Husa-. . . huchukua . . . Na hilo ndilo linalosababisha homa kutoka kwenye ambukizo. Huchukua ambukizo na—na kusababisha homa.

34 Naam, hao watu, mnaona, ni imani yako. Si kujisikia kwako kamwe. Si kitu, kama ndivyo ilivyo, kama mkono wangu haukunyoka. Hilo halina uhusiano wo wote nalo. Imani yangu ndiyo inayofanya jambo hilo. Mnaona? Papa hapa mbele yetu, tunaona mfano wa mtu aliyeponywa kabisa, kwa imani. Kisha tunapiga hatua kwa hatua hata tutakapomfikia mtu huyo, kisha tunatembea moja kwa moja nayo. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo. Na hilo, hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, imani yako. Si kujisikia kwako. Imani yako hutenda hilo. Shukrani na sifa ziwe kwa Mungu!

35 Sasa dakika moja tu ya maombi, nasi tuna somo hapa ambalo tunataka kulitilia maanani, na wakati mdogo ambao Bwana angeshughulika nasi kulingana na jambo hili.

Basi, sasa, halafu kama wengine wenu hawana budi kwenda zao asubuhi ya leo, nao hawatakuwa kwenye ibada ya jioni, Bwana akipenda, na—nataka kuwa hapa tena. Jamaa yangu inarudi kwenye juma la Krismasi. Halafu basi, Jumapili baada ya Krisimasi, Bwana akipenda, nataka kuhubiri Ujumbe wangu wa Krisimasi hapa kwenye Maskani; Jumapili inayofuatia Krismasi. Bwana akipenda, somo litakuwa, *Mzururaji Barabarani.*

Kwa hiyo hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa tuombe dua kabla hatujasoma hilo fungu la maneno.

36 Bwana Yesu, uwe karibu nasi wakati huu. Nasi tunajua ya kwamba ni vigumu katika kanisa letu dogo, na wakati wengi wanaposimama. Na—nasi tuko hapa si kwa sababu ya starehe ya mahali hapa, ambapo panatupa burudiko la kimwili, kwa maana hapaburudishi. Nasi hatuko hapa kuonekana. Bali tuko hapa kwa sababu tulisikia Uwepo Wako. Nasi tunajua ya kwamba Wewe uko hapa. Nasi tuko hapa kwa ajili ya kusahihishwa. Nasi tuko hapa, tukijua ya kwamba tuko katika nyumba ya Mungu. Nasi tunajisikia vizuri kuwa hapa, haidhuru panakalifu namna gani, huko kusimama, na—na kuketi mmesongamana,

bali tuko hapa kwa sababu kwamba tu—tunajisikia kwamba Mungu yuko hapa.

37 Na vivyo hivyo hapana budi ndivyo yule mvulana alivyojisikia usiku ule, wakati Paulo alipohubiri usiku kucha, ni ujumbe mrefu jinsi gani, kutoka labda machweo ya jua hata kuchomoza kwa jua, asubuhi iliyofuata. Naye huyo mvulana mdogo akiketi kule juu kabisa, alianguka nao wakafikiri kwamba amekufa. Ndipo Paulo akaweka mwili wake juu yake, na Roho wa Mungu aliyekuwa juu ya yule mjumbe akairudisha roho ya uzima kwenye mwili wa huyo mvulana. Ndipo akasema, “Atakuwa sawa,” basi huyo kijana mwanamume akaishi. Aliyapenda yale Paulo aliyokuwa anasema.

38 Basi, Mungu, tunapenda asubuhi ya leo kile Roho Mtakatifu angenena katika mioyo yetu. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utammegea kila mmoja wetu Mkate wa Uzima, ili kwamba tutakapoondoka hapa leo, kwamba hatutaliacha jengo hili watu wale wale tuliokuwa tulipoingia. Wajalie Wakristo wawe karibu Nawe zaidi. Jalia wenye dhambi wageuke leo. Wagonjwa na waponywe. Pia jalia Ufalme wa Mungu uje karibu nasi, ama hata uwe ndani yetu. Kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu Kristo, tunapomngojea Roho Wake atupe Maneno. Amina.

39 Basi hebu tusome baadhi ya Maandiko, ambayo ni . . . Neno la Mungu daima ni sahihi.

Na sasa, na kila mmoja, naona ninyi mna huruma sana kwa wale wanaosimama. Namwona mtu akisimama na kuketi chini, na kumpa mtu mwingine kiti. Hilo ni jambo zuri sana. Laiti tungalikuwa na nafasi zaidi, bali hatuna kabisa, wakati huu.

Fungueni Mathayo 27, nasi tutasoma kutoka aya ya 11, kisha tutazungumza juu ya somo hili.

> *Naye Yesu akasimama mbele ya liwali: liwali akamwuliza, akasema, Wewe ndiwe Mfalme wa Wayahudi? Yesu akamwambia, Wewe wasema.*
>
> *Lakini aliposhitakiwa na wakuu wa makuhani na wazee, hakujibu hata neno.*
>
> *Ndipo Pilato akamwambia, Husikii ni mambo mangapi wanayokushuhudia?*
>
> *Asimjibu hata neno moja, hata liwali akastaajabu sana.*
>
> *Basi wakati wa siku kuu, li—liwali desturi yake huwafungulia mkutano mfungwa mmoja waliyemtaka.*
>
> *Basi palikuwa na mfungwa mashuhuri siku zile, aitwaye Baraba.*
>
> *Basi walipokutanika, Pilato akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi? yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo?*

*Kwa maana alijua ya kuwa wamemtoa kwa husuda.*

Na *alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, Usiwe... na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake.*

*Nao wakuu na makuhani na wazee wakawashawishi makutano ili wamtake Baraba, na kumwangamiza Yesu.*

*Basi liwali akajibu, akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi katika hawa wawili?...*(Wazia jambo hilo!)...*Wakasema, Baraba.*

*Pilato akawaambia, Basi, nimtendeje Yesu aitwaye Kristo? Nimtendeje Yesu aitwaye Kristo?* Ndipo *wakasema wote, Asulibiwe.*

*Akasema, Kwani?...ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, wakisema, Na asulibiwe.*

Basi *Pilato alipoona ya kuwa hafai lo lote, bali ghasi inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe.*

*Watu wote wakajibu wakasema, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.*

*Ndipo akawafungulia Baraba; na baada ya kumpiga Yesu mijeledi, akamtoa ili asulibiwe.*

40 Ni picha ya huzuni namna gani! Ninaita fungu la hili, kama mnataka kuliandika namna hiyo, ama kuliita hivyo. Na labda kanda ingetaka kuitwa hivi: *Nimtendeje Yesu Aitwaye Kristo*? Na somo ninalotaka kutumia, baada ya hilo kuwa ndilo fungu la maneno; ninataka kutumia somo, "ukiwa na Yesu mikononi mwako." Ukiwa na Yesu mikononi mwako, utafanya nini?

41 Tamasha letu linaanzia, asubuhi ya leo, kwenye ukumbi wa mahakama; ambapo Pilato, yule liwali, alikuwa ameitwa jukwaani, ku-kutenda na—na kutoa hukumu. Ilikuwa asubuhi na mapema, muda kidogo kabla ya mapambazuko, naye alikuwa amesumbuliwa akaamka, na—na alikuwa ameitwa kusikiliza ke—kesi ya Mtu huyu.

42 Ilikuwa ni wakati wa kusulubiwa kwa Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Ha—hakuwa amefanya kitu, walichoweza kupata, Naye alikuwa—Naye alikuwa amejibu kila kitu. Ilikuwa tu ni saa ambayo mambo yalibidi kuwa namna hiyo.

Hakuna cho chote kinachoweza kutendeka bila ya kuwa na kitu fulani nyuma yake kukisababisha kuwa hivyo. Hapana budi kuwe na sababu fulani kwa kila kitu kinachotendeka. Kwa kuwa ki—kinasababishwa, bila shaka, na ro—roho aliye ndani

ya viumbe, na katika wanadamu, na kadhalika. Kuna kusudi, kusudi lake, na—na shabaha, na hapana budi kuwe na sababu.

Nalo, sababu ya jambo hili kulazimika kumpata Mtu huyu mkuu kuliko wote aliyepata kuishi duniani, ama ambaye angewahi kuishi; sababu ya jambo hilo kutukia kwa njia hii, ni kwa sababu ilikuwa ni wakati wake wa kutukia. Mnaona? Haina budi kuwa hivyo, wala hapakuwepo na njia ya kuepuka jambo hilo. Nalo, ilibidi litimie wakati huo.

Naye Yesu alikuwa amekuja duniani jinsi vile hasa Neno la Mungu lilivyokuwa limebashiri Yeye angekuja. Yeye alifanya vile vile hasa Neno lilivyosema Yeye angefanya. Yeye aliishi hayo maisha, kikamilifu kabisa, ndipo Mungu akamtambulisha, ama akamdhihirisha, yule Mzao wa wakati ule. Sasa kumbukeni, Mungu . . .

43 Biblia inaanza katika Mwanzo na kuendelea hadi Ufunuo. Sasa hili hapa somo ambalo na—nawatakeni mfahamu, kwamba . . . Mnaona, katika kila kizazi imekwisha nenwa, katika Biblia, juu ya jambo fulani kutukia katika kila kizazi.

Kama vile Danieli alivyoona lile . . . alivyofasiri ndoto ya Nebkadreza; jinsi falme za Mataifa zingeingia, na jinsi gani zingeanguka, na jinsi gani zingekwisha. Na kila mmoja wa watu hao katika jamii hizo na mataifa hayo, hizo nguvu za Kimataifa zinazotawala, zimeutawala ulimwengu, zimefanya vile vile kabisa ambavyo lile ono lilisema zingefanya.

44 Wakati Nebkadreza, kile kichwa cha dhahabu, alipoondoshwa, basi Wamedi-Waajemi wakaingia; na tabia yao, kulingana na—na hali ya vile vitu, na kulingana na vile alivyosema nabii, barabara kabisa. Nebkadreza, kichwa cha dhahabu, ambao ndio mkubwa kuliko zote na wa kwanza wa ule Ufalme. Basi ule wa Wamedi-Waajemi ukiwa wa fedha. Halafu moja kwa moja mpaka kufikia kwenye mapaja, ya—ya shaba. Na kila madini yanazidi na kuzidi kuwa magumu; dhahabu ikiwa ndiyo laini kuliko yote. Na inaishia katika chuma, ambacho ndicho kigumu kuliko hayo yote, ni chuma.

Naam, kila moja ya falme hizo zilikuja kikamilifu kabisa, kwa tabia, jinsi ambavyo nabii alisema kwamba zingefanya. Naye alikuwa anafanya nini? Alikuwa akipanda mbegu kwa ajili ya mataifa kusudi waangalie, na kila wakati ambapo huo ufalme ulianzishwa, ilibidi utende kulingana na vile lile Neno lilivyosema.

45 Na halafu Masihi ilibidi ajitokeze hadharani. Basi Kristo alipojitokeza hadharani, ilimbidi ajibu hayo Maneno ya Mungu yaliyokuwa yatimizwe, ambayo nabii alinena juu yake, yale ambayo Yeye angefanya.

Musa alisema, “Yeye atakuwa—Yeye atakuwa Nabii kwa mithili yangu.” Na kama mngekuwa . . . tungalikuwa na wakati wa kufananisha hilo huko nyuma na kuonyesha tu jinsi ambavyo

katika wakati ule muhimu sana, wakati Israeli walipokuwa utumwani huko Misri, jinsi ambavyo Musa alivyozaliwa akiwa mtoto wa kipekee na maalumu; na jinsi ambavyo a—alikuja, na akalelewa, na jinsi alivyofichwa kwenye manyasi; na jinsi alivyokuwa kiongozi, akaenda milimani akapata zile amri, kisha akashuka chini. Wala hakuwa kiongozi tu; bali alikuwa kuhani, na mfalme, na liwali. Mambo hayo yote, na jinsi ambavyo jambo hilo lilimfananisha Kristo kikamilifu kabisa. Naye Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii aliye mithili yangu." Mnaona?

46 Naam, wakati Yesu alipozaliwa, Israeli ilikuwa tena katika utumwa wa Dola ya Kirumi. Naye alikuwa nini? Alizaliwa Mtoto maalumu, na wa kipekee, na jinsi alivyolelewa. Jinsi alivyopanda milimani, kisha akashuka akasema, "Mmewasikia wakisema, wao wa hizo nyakati za kale, 'Usiibe.' Mmewasikia wakisema, 'Usizini,' lakini Mimi nasema, yeye amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amefanya uzinzi tayari." Mtoa Torati, mnaona, na Mfalme, Kuhani, Nabii, kama yeye hasa. Kwa hiyo mambo haya yote yalipaswa kutimizwa, na wakati kipindi hicho kikidumu pale kwa ajili ya maisha ya Masihi, wakati jambo hilo lilipothibitishwa kikamilifu.

Naam, hili laweza kuwa ndilo somo refu la mwisho nitakalofundisha kwa kitambo kidogo. Nawatakeni mlifahamu vizuri sasa.

47 Wakati Neno limekwisha kunenwa kwa ajili ya kizazi hiki fulani, kutakuweko na mtu atakayejitokeza hadharani ambaye atalitimiza Neno hilo, kwa maana Mungu amekwisha linena. Ni kuthibitishwa kwa Neno lililonenwa. Naye Yesu alitimiza kila sifa, naye alikuwa Neno, amethibitishwa kama Masihi, hasa. Kuna Maneno pia, yaliyonenwa katika Biblia, kwa ajili ya siku ya mwisho. Hayo maneno hayana budi kuwa hai.

48 Nasi tunaona hapa ya kwamba, wakati katika siku za Bwana wetu, kanisa tayari lilikuwa limemkataa Yeye kabla hajaja kwenye ukumbi wa hukumu wa Pilato. Wao walikuwa wamemkataa, tangu siku ile huduma yake ilipoanza kutabiri na kuwaambia wao Kweli juu ya Neno. Halafu, wao hawakuweza kuelewa na jambo hilo, jinsi Yeye, akiwa Mwanadamu, angalijua kilichokuwa ndani ya mioyo ya watu. Hawakujua hata kidogo, ya kwamba, Neno ni Mungu! "Nalo Neno," Biblia ilisema, "huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

49 Nao walitaka kumwita Yeye pepo mchafu. Ndipo Yeye akasema, "Nitawasamehe kwa ajili ya jambo hilo. Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, kusema neno juu Yake hamtasamehewa kamwe."

Na mambo haya yote aliyotabiri yatakuwako katika siku hii, kitu fulani hakina budi kuyahuisha hayo. Lakini wakati Hilo linapofanywa hai, litakuwa tofauti sana na vile watu

wanavyofikiri lilivyo, mpaka ita—itakuwa tu ni Walio Wateule watakaoona jambo Hilo. Daima, Wateule tu ndio pekee watakaoliona Jambo Hilo, kwa maana Wao wameteuliwa na kuchaguliwa kuliona Hilo. Kwa hiyo, haiwezekani, hakuna njia nyingine.

50 Yesu alisema, "Hamwezi kuja Kwangu. Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu; nao wote alionipa Yeye watakuja Kwangu." Mnaona? Mnaona? Kwa hiyo hakukuwa na njia. Yeye alisema, "Mna macho na hamwezi kuona; maskio, hamwezi kusikia." Kasema, "Isaya alitabiri vema juu yenu." Mnaona? Unabii wa Isaya ukizuka, ukidhihirishwa.

Msisahau jambo hilo, hapa ama anayesikiliza kanda, ya kwamba Neno la Mungu halina budi kudhihirishwa. Mungu anawajibika kuona kwamba Hilo linafanya hivyo.

51 Kama tu vile Yohana Mbatizaji alivyochaguliwa hapo awali kutangulia kuja kwa Kristo, ilibidi kuwe na mtu fulani atakayeinuka kupachukua mahali hapo. Neno hilo lilikuwa halina budi kutimizwa.

52 Ndipo Yesu alipokuja kama Masihi aliyetiwa mafuta, na kufanya vile vile kabisa ambavyo Neno la Mungu lilisema angefanya; na hata hivyo Wayahudi walikuwa wakitazamia jambo lingine, "Mfalme ajaye na fimbo ya chuma mkononi Mwake," jambo ambalo lilikuwa la siku za usoni kabisa. Bali Yeye alitimiza kila Neno.

Pale siku moja huko Kapernaumu, wakati alipoyatwaa Maandiko na kusoma, (mliona?) Yeye alisoma tu sehemu ya Maandiko hayo. Ndipo akakiweka Kitabu chini na kusema, "Leo haya yametimizwa."

53 Wakati alikuwa ahubiri mwaka wa yubile, basi, kwa nini Yeye hakusoma yale mengine? Kwa maana Hilo linahusu kule Kuja Kwake kwingine. Wao hawakuwa na haja ya kujua jambo hilo. Hilo ni kwa wakati atakapoingia.

Lakini wakati alipoingia, hiyo ndiyo sababu Yeye aliweza, "Maandiko haya yametimia leo machoni mwenu. Papa hapa mnaliona. "Kuhubiri majira yaliyokubalika, na kuwafunga waliovunjika moyo, na kuwaponya wagonjwa," hayo ndiyo aliyoyajia.

Yaliyosalia yalikuwa—yalikuwa kutoa hukumu kwa Mataifa, na kadhalika, kwa hiyo jambo hilo linafuata. Mnaona, Mataifa yalipaswa kumkataa Yeye, kwanza.

54 Naam, kwenye kule kusulubishwa, mahali tulipo leo kwenye hili somo, la, "Yesu mikononi mwako." Neno la Mungu lilikuwa limethibitishwa kabisa, lilikuwa limehakikishwa tena na tena, ya kwamba Yeye alikuwa jibu la Neno la Mungu. Mahali ambapo Waandishi . . .

55 Mnaona, Mungu tayari ameliweka wazi. Hebu huduma ijifunze Hilo. Lakini, mnaona, wao wanachukua neno la mtu mwingine kuhusu jambo Hilo; kundi fulani la mtu. Wao wamepofushwa sana kwa ile Kweli, hata, wakati Kweli inapoonyeshwa wazi, wanakosa kuiona. Lakini, mnaona, Mungu ni mwenye haki, Yeye ameliandika kule. Yeye ameliandika, papa hapa kwenye Kitabu, kile kitakachotendeka leo, kwa hiyo jambo Hilo litatimilizwa. Bali wengine ambao hawakukusudiwa kuliona Hilo, hawataliona kamwe, mnaona, wao—wao wamelichanganya lote.

56 Na hivyo ndivyo walivyotenda jambo Hilo wakati huo. Wao hawakuwa wamejua kamwe kwamba ni Yeye. Na kwa ishara ya kwamba Yeye alikuwa Mjumbe wa wakati huo, hakuna mtu angaliweza kukanusha jambo hilo. Nabii Wake alinena juu ya jambo hilo; alisema, “Mimi, sina budi kupungua, bali Yeye atazidi. Mimi sistahili kuvilegeza viatu vyake, bali Yeye anasimama kati yenu sasa,” kasema Yohana. “Naye atakuja. Nalo shoka limewekwa penye shina la mti; na miti isiyozaa matunda itatolewa mwituni, hata, ama kutoka kwenye sha—shamba la mizabibu, ama sha—shamba la matunda. Haitakuweko tena.”

57 Naam, tunaona ya kwamba mambo hayo yalitukia jinsi tu Yeye alivyosema. Yeye angeweza kutambua mawazo yao moyoni mwao. Alikuwa nabii. Kila alichotabiri, kilitukia sawasawa tu na jinsi Yeye alivyosema.

“Ninapanda kwenda Yerusalemu. Huko nitawekwa katika mikono ya watu wenye dhambi. Nao watamtenda vibaya, kisha atasulubishwa. Na katika siku ya tatu atafufuka tena.” Lakini kasema, “Msimwambie mtu ye yote jambo hili.” Naye akawapofusha kwa jambo Hilo, hata hawakulielewa mpaka Hilo lilipotimizwa.

58 Mnaona, mara nyingi ambapo Yeye anatuacha tuwe vipofu mpaka saa ile tunapohitaji jambo Hilo. Yeye anatuacha tuwe vipofu kwa mambo tunayoyaona leo, kwa maana hii ndiyo saa tunayohitaji, kuthibitisha siku tunamoishi. Mnaona? Baba zetu hawakujua mambo haya. Biblia ilisema ya kwamba wasingeyajua. Yeye alikuwa amewaficha, na katika—katika siku za mwisho yangefunuliwa kwa wana wa Mungu; ama, kufanya, yangedhihirishwa, kuonyesha utukufu Wake na sifa Zake juu ya nchi.

59 Na yote yale aliyosema Danieli juu ya siku za mwisho, na jinsi ambavyo, “Hao wamjuao Mungu wao watafanya mambo makuu.” Na Maandiko mengi sana yakishikana katika siku hii ya mwisho tunayoishi! Na jinsi ambavyo nyakati hizi mbovu na za udanganyifu zingekuwepo duniani. Na jinsi hasa mambo tuliyo nayo sasa yanatimiliza jambo Hilo.

Wao, walikuwa—walikuwa wamepewa nafasi ya kumwona Yeye, na, lakini wao walimkataa yule Masihi wao.

Na leo ni jambo lile lile, jambo lile lile. Tunapewa nafasi, kwa maana Mungu hawezi kuhukumu bila kwanza kuwa . . . kuwa mwenye haki kwa hukumu Yake.

Naam, kama ungemwambia mtu fu—fulani akienda zake barabarani, akienda kasi; ungewasimamisha, useme, "Kuna shimo kule chini barabarani. Kama ukiendelea na mbio hizo, utakufa."

60 Nao wanasema, "Upuzi, ninajua ninachofanya." Basi, unaona, hiyo damu haiwezi kuwa juu yako, kwa maana umewaonya sana.

Vema, Mungu hufanya jambo lile lile kwa Neno Lake. Yeye huwaonya watu sana juu ya hukumu inayokuja, na kuonyesha ishara Zake na maajabu yaliyobashiriwa katika Biblia kwa ajili ya wakati huo. Yeye huwaonyesha, nao watu wanatembea moja kwa moja juu Yake.

Si rahisi kwa mtu kwenda jehanamu. Mtu hupigana na njia ya kwenda jehanamu. Uongo wa kwanza uliowahi kusema, unajua ulikuwa ni kosa. Sigara ya kwanza uliyopata kuvuta, ulijua ilikuwa ni kosa. Uovu wa kwanza uliofanya, ulijua ulikuwa ni kosa. Lakini katika dhamiri yako, ilikwambia ilikuwa ni kosa, bali uliendelea kukimbia ukavuka ile taa nyekundu, ukavuka vizuizi. Wewe hujali. Unataka kufanya jambo hilo, hata hivyo, kuonyesha kwamba wewe ni jamaa mashuhuri. Mnaona? Lakini, kumbuka, unapigana na njia ya kwenda jehanamu. Si rahisi kwenda jehanamu. Inakubidi kuikataa ile Kweli.

61 Kabla hujapatwa na ajali, huna budi kwenda kasi uvuke ile taa nyekundu. Kabla hujapatwa na ajali, wewe huna budi, huko barabarani, una i—ilani ambazo zimewekwa. Lakini, wewe, una njia yako juu ya jambo hilo, mwanadamu anayo leo. Naye anajua zaidi ya mtu mwingine ye yote, wala hatazisikiliza i—ishara na ilani za Hukumu inayokuja, na wale wanaomkataa Kristo.

62 Sasa angalia, na kile walichokuwa wamekubali badala ya Kristo huyu. Sasa wazia juu ya kanisa la siku hiyo, upofu wao. Wao walikuwa wamemkataa muuaji wa waziwazi, Baraba. Mtu aliyekuwa amethibitishwa kuwa muuaji, naye alikuwa kweli akingojea hukumu yake. Na—naye alikuwa amethibitishwa ku—kuwa muuaji, tena alikuwa mtu mbaya. Na kwa sababu tu ya kwamba—kwamba Maisha ya Yesu . . .

Ambayo, Yeye, Yeye aliwasai. Alisema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunishuhudia Mimi ya kuwa nina dhambi?" *Dhambi* ni "kutokuamini." "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini; kama sijawaambia Kweli ya Maandiko. Nayo Maandiko yamenena habari Zangu, Yenyewe. Mwayachunguza Maandiko," Yeye alisema, "kwa sababu mnadhani kwamba

ninyi mna Uzima wa Milele ndani Yake, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia katika wakati huu."

63 Lakini wao walisema, "Anajifanya Mwenyewe Mungu. Anajifanya Mweneyewe kitu fulani." Hakufanya kitu . . . Mungu alimfanya Yeye Mungu; Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa ni kutimizwa kwa Maandiko. Yeye hakujifanya kitu cho chote. Mungu alimfanya kile alichokuwa. Halafu, basi, ilikuwa ni kwa sababu ilikuwa saa ya Neno hilo kutimizwa. Kwa hiyo, bali wao hawakuweza kuona jambo Hilo, kwa maana ilikuwa ni kinyume cha mawazo yao ya kimadhehebu, kile walichokuwa wamejenga kuhusu Kristo. Nalo lilikuwa limepofushwa sana kutokana na Neno.

64 Naam, na mbali na jambo hilo, kumwondolea mbali Jamaa huyu, iliwabidi kumkubali muuaji, kitisho kwa watu, pia. Ilikuwa ni hasara kwa umma, hasara kwao; muuaji! Iliwabidi kumkubali huyo, kwa sababu, ku—kumkataa Kristo.

Na kabla ya mwanamume ye yote ama mwanamke ye yote kuweza kukubali mabaya, hawana budi kukataa mema. Kuna kitu fulani kuhusu maumbile, yana kanuni zake, kwamba huna budi kukataa jambo lililo sahihi kabla hujapokea jambo lililo makosa.

Kama tu nilivyonukuu hivi punde, ku—kuacha kusema uongo . . . U—ulisema uongo dhidi ya uamuzi wako mzuri. Ulisema uongo dhidi ya dhamiri yako. Ulisema uongo dhidi ya yale mama yako ama wazazi wako walivyokufundisha kufanya. Ama, hata maumbile yenyewe yanakufundisha usifanye hivyo. Kwa hiyo, basi, wewe, kuikataa Kweli, huna budi kukubali u—u—uongo, nawe huna budi kukataa Kweli kabla hujaukubali uongo. Mnaona?

65 Kwa hiyo hivyo ndivyo jamaa hawa walivyokuwa wamefanya, walikuwa wameikataa ile Kweli. Naye alikuwa ndiye ile Kweli. "Mimi ndimi Njia, Kweli na Uzima."

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akadhihirishwa mbele zetu." Katika Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akashikwa kwa mikono yetu." Mungu, Yehova! Ni—ni jambo la kushangaza sana, ni la kuogofya sana, kufikiri ya kwamba Mungu aliyeweka mfumo wa jua na sayari zinazolizunguka angani, aliyefanya nyota ambazo ni kubwa kuliko dunia hii mara elfu moja . . .

66 Na kama moja ya hizo nyota ingeanza kuja duniani, kwa mwendo wa maili elfu kumi kwa saa, mbona, ingechukua miaka milioni mia moja kufika hapa; iko mbali sana. Na nyota mbili ndogo zilizokaa, zinazoonekana kama zimeachana kwa inchi moja, kutoka hapa, ziko mbali sana moja kwa nyingine kuliko sisi tulivyo mbali nazo. Na, hata hivyo, hakuna hata moja ya

hizo isiyoshikilia mahali pake. Na jamii hiyo kuu ya nyota, loo, jamani, wingi na ukubwa wa Mungu Ambaye angefanya mambo hayo! Kila moja haina budi kushikilia ile nyingine. Hiyo ndiyo sababu zinakaa jinsi zinavyokaa. Kama zikitoka mahali pao, mfumo wote ungevurugika.

67 Basi hivyo ndivyo ilivyotukia Edeni. Wakati Hawa alipotoka mahali pake juu ya amri za Mungu, jamii yote iliangauka.

Hiyo ndiyo shida leo. Haitupasi kuvurugika katika mashirika na madhehebu, na kadhalika. Inatupasa kuwa wana na binti za Mungu, tukishikilia ile jamii kuu ya nyota za ulimwengu pamoja.

68 New York, juma lililopita, nilikuwa nikisikiliza ujumbe ulionukuliwa, ama kunenwa na Einstein, yule mwana sayansi mashuri sana, yule—yule anayeitwa bongo la—la wakati huu. Nami nilikuwa. . .niliusikia huo. Kisha nikaenda kumsiliza Norman Vincent Peale, katika saikolojia yake juu ya jinsi watu wanavyopaswa kufanya, ama kuenenda, na kujiendeleza katika saikolojia.

Basi, juu ya Einstein, yeye alikuwa akizungumza juu ya kundi la nyota lililokuwa kule katikati ya ule mfumo kule, huko nje mbali na zilipo nyota. Basi kama mtu angaliweza kwenda katika mwendo, naamini alisema, wa nuru,. . . Naam, nafikiri, ni upi huo,. . .elfu themanini na sita? [Ndugu Neville anasema, "Mia moja themanini na sita elfu."—Mh.] Mia, mia na themanini na sita elfu kwa sekunde, ambayo nuru huenda. Na sasa vunjavunja huo katika dakika tano, ungekuwa mamilioni na mabilioni mangapi ya maili. Basi ingechukua miaka mia—mia na ishirini elfu ya wakati wa nuru kufikia lile kundi la nyota. Halafu miaka mia na ishirini, ama miaka milioni mia na hamsini elfu; miaka milioni mia moja na hamsini kwenda, kisha miaka milioni mia moja na hamsini kurudi.

69 Ndipo wao wakafikia kitu kilichowatatiza. Nao, baada ya kwenda kule na kurudi, ungekuwa tu umechukua miaka milioni tatu kufanya hiyo safari, miaka milioni mia tatu. Miaka milioni mia tatu kufanya safari hiyo, na, ukirudi duniani, kweli umesafiri tu miaka hamsini. Unaingia katika Umilele. Hamna mwisho Wake.

70 Basi kuwazia, ya kwamba, Mungu aliyeumba hayo yote na kuyaweka katika utaratibu, na kuyanena, alishuka na kufanyika mwili kati yetu, kutukomboa. Naye angetuheshimu sana kwa Uwepo Wake wenye utukufu, hata Yeye—Yeye angesimama hapa juu ya dunia hii yenye dhambi katika siku za mwisho, na kuthibitisha Neno Lake kuwa hivyo, kwa maana Yeye anawajibika kwenye hilo Neno. Amina. Ukuu na haki ya Huyo Mkuu ambaye anashikilia mambo hayo katika mkono Wake!

71 Angalia, mataifa. Ka—kanisa halina budi kulikataa Neno Lake, kwanza. Kisha, baada ya kanisa kulikataa, na kumwita

"Beelzebuli, ama pepo mchafu," ndipo Hilo likaletwa mbele ya serikali, ili kwamba jamii yote ipate kuhukumiwa. Basi tunamwona Yesu, asubuhi hii, mbele ya—ya liwali, Pilato, Mrumi, ili ahukumiwe. Nasi tunaona kwamba kanisa lilimkataa, kwanza, kwa sababu wao hawakuuamini Ujumbe Wake, kwa sababu wao hawakulijua Neno.

72 Yesu aliwaambia, "Kama mngali—mngalimsikia Musa, mngeliliamini Neno Langu, kwa maana yeye ndiye aliyenena habari Zangu." Mnaona? Hilo hapo Neno ambalo nabii... Ambalo, Bwa—Bwana humjia nabii, naye nabii alinena Neno kwa ajili ya wakati wa usoni. Kisha hapa likatambulishwa, na kusema, "Mnasema mnamjua Musa naye ni kiongozi wenu. Hammjui Musa, wala hamjui Neno lake." Kwa maneno mengine, Yeye alisema, "Mimi ndiye hilo Neno. Mimi ndiye Hilo Neno lililotambulishwa ambalo Musa alisema litakuja, nanyi mnanihukumu Mimi." Mnaona? Kwa ajili ya mapokeo yao, mnaona, kanisa lilimhukumu Yeye.

73 Naam, tunamwona sasa mbele za Pilato, na amehakikishwa kabisa, pia, ametambulishwa kwa huo wakati, ama kanisa, na mjumbe wa wakati. Wao walikuwa wamepewa nafasi kuona na kuamini Hilo; bali wakalikataa. Kwa nini wakalikataa? Wengi wao walitaka kuamini jambo Hilo; lakini mapokeo yao, si hao watu, ila mapokeo yao!

74 Naam, mnaona, kama vile Nikodemo alivyokuja usiku, naye akasema, "Bwana, twajua kuwa U mwalimu aliyetoka kwa Mungu. Tunajua ya kwamba Wewe unatoka kwa Mungu. Hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya uyafanyayo isipokuwa Mungu awe pamoja Naye. Sisi..." Hao "Sisi" anayenena habari zao ni akina nani? Kanisa, Mafarisayo, viongozi wa wakati huo. "Tunajua. Sisi tumeshawishika kabisa ya kwamba Wewe ndiye Mtu huyo." Kwa nini basi wao wasingeweza kutenda jambo hilo? Kwa sababu, madhehebu yao. Ninataka hilo likolee ndani kabisa, kwa maana hilo ndilo ninaliendea. Mnaona? Madhehebu waliyokuwa wamejiunga nayo, ndiyo ambayo wasingeweza kutoka. Ingawa waliona ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, lakini madhehebu waliyokuwa wanahusika nayo yasingewaruhusu kuliamini.

Mna—mnafahamu? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Sasa nataka kuuliza, kutoka kwenye wasikilizaji hawa wanaoonekana, ni wangapi wanaofahamu ninachonena habari zake? Inueni mikono yenu. Vema.

75 Naam, madhehebu! Waliliamini Hilo, nao walijua lilikuwa Ndilo. Jinsi ningetaka kusema jambo lilo hilo leo! Tunaona kile kinachopaswa kuwa hapa leo, nasi tunaliona, bali madhehebu hayatawaruhusu kukubali jambo Hilo. Wao wameshikwa sana na madhehebu hayo! Mnaona, si huyo mtu, ni hayo madhehebu.

Kama tu vile nilivyonena juu ya Rais ambaye ameuawa hivi punde. Si huyo mtu; nijuavyo mimi, yeye ni mtu mzuri, hajafanya lo lote baya kama nijuavyo mimi. Bali ni yale madhehebu. Si hao watu; ni madhehebu.

76 Haikuwa ni Wayahudi; ilikuwa madhehebu yao. Madhehebu hayo yalimhukumu Yeye, kwa kuwa Hilo halikuvumiliana na madhehebu yao. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, mambo yale yale yanatukia sasa. Nao walimchagua huyu adui wa umma, muuaji.

Lakini kisa hicho sasa kimekwisha kuihusu serikali. Kwa hiyo serikali haina budi kutoa hukumu hii, kwa sababu, kutoa uhai, lazima jambo hilo lifikishwe mbele ya serikali. Wao hawakuwa wamekubaliwa kufanya jambo hilo, kwa maana walikuwa chini ya u—utawala wa Rumi, nao wasingeweza kutoa uhai haidhuru kanisa lao lilisema nini, "Hatuna budi kufanya jambo hilo." Mbona, wao—wao wasingefanya jambo hilo bila, kwanza, Rumi kuwapa kibali cha kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, hakina budi kuletwa mbele ya serikali. Sasa serikali inahusika katika kisa hicho.

Naam, kama jambo hilo si picha ya leo, sioni ni kitu gani. Mnaona, sawa kabisa!

77 Kanisa linalikataa, sasa ni serikali inahusika. Wakati ulikuwa umewadia ambapo taifa, la wote, lote, lilipaswa kuja. Kisa kililetwa. Shindano la kuamua lilikuwa limewadia. Taifa zima lilikuwa limemkataa, na kushusha hasira ya Mungu juu yao. Na kabla ya . . . Hata kanisa lilikuwa limemkataa, jambo ambalo lingeshusha hasira ya Mungu juu ya kanisa. Lakini sasa taifa limemkataa Yeye, ili kuileta hasira juu ya wote.

Basi, leo, ulimwengu umemkataa Yeye, kuleta hukumu juu ya ulimwengu wote. Mataifa yote hayana budi kuhukumiwa.

78 Basi tunajua ya kwamba jambo hilo lilitukia katika wakati wa yule jenerali mkuu wa Kirumi, Titus. Yeye aliuzingira Yerusalemu, kisha hatimaye akanini hii tu . . . Wao waliwala watoto wao wenyewe kwa wenyewe; wakala maganda toka kwenye mti, na nyasi kutoka ardhini. Ndipo—ndipo basi Titus akaingia moja kwa moja na akazibomoa tu kuta na kuuteketeza ule mji kwa moto, ndipo damu ikatiririka—ikatiririka barabarani namna hiyo, ambapo alikuwa amewaua mle ndani.

Na ilipaswa iwe namna hiyo. Kabla Mungu mwenye haki hajawaacha watu, ambao alikuwa amewachagua, kuja chini ya kitu kama hicho, hapana budi pawe na sababu ya haki. Yeye ni mwenye haki. Yeye ni. She—sheria Zake zilihitaji haki Yake. Wala sheria isiyo na adhabu si sheria.

79 Kama ningesema, ningetunga sheria hapa mjini, "Ni fa—fa—faini kuvuka taa nyekundu," halafu kusiwe na adhabu

kwa jambo hilo, ungeendelea tu kuvuka taa nyekundu. Lakini hakuna budi kuwe na adhabu.

Na adhabu ya sheria ya Mungu, kukataa mpango Wake, ni mauti. Na ilibidi kuwe na mauti, kwa hiyo ilibidi ilipwe.

80 Tunasimama kwenye hukumu ya namna ile ile asubuhi hii, ulimwenguni kote, shtaka. Madhehebu yote yamelikataa Neno. Najua hili linasikika kali sana. Nami nawataka wahudumu wanaosikiliza, walioko hapa na wale walio kwenye kanda, pia, kujaribu kufahamu jambo hili sasa, ambalo ninajaribu kulifanya dhahiri. Bali ninashikilia maoni yangu, ama ninatoa maoni yangu hapa, na kusema kwamba tunasimama, leo, [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara tatu—Mh.] katika ukumbi mwingine wa hukumu wa Pilato.

81 Unasema, "Kama ningalikuwa nimesimama pale, ningalimtetea Yesu Kristo." Na, sasa, unafanya nini kuhusu jambo hilo sasa hivi? Jambo ndilo hilo. Unaona? "Haidhuru kiasi gani kanisa lilikuwa limemkataa, ningalisimama upande Wake." Wewe unayo nafasi. A-ha. Unaona? Wao, wao walimkataa.

82 Sasa Yeye anahukumiwa, leo, ama ndiyo kwanza ahukumiwe, ama, na yuko hukumuni, ili kwamba shirika la ulimwengu liundwe, la kile kinachoitwa, halmashauri ya makanisa, ku—ku—kuundwa katika—katika Baraza la makanisa Ulimwenguni. Naam, nao wamefanya nini? Wao wamepiga kura ya kwamba kabisa wataungana pamoja na kuwa na baraza la makanisa.

Na katika Baraza hili la Makanisa, kwamba makanisa yote hayana budi kuwa wanachama wa baraza hili, la sivyo, kama hawatakuwa, hata huruhusiwi hata kuhubiri, huruhusiwi hata kuwaombea wagonjwa. Na kanisa lenu linaweza kutumiwa kwa jambo lo lote wanalotaka kulitumia kwalo. Kama wanataka kuweka makasha ndani yake, ama zana za vita, ama cho chote wanachotaka kufanya, huna mamlaka nalo kamwe. Aidha wewe ni mfuasi wa Baraza la Makanisa au wewe hu mfuasi kamwe.

Basi hilo ndilo shirika lililoundwa hapa Marekani, ambalo linatimiza Maandiko, kikamilifu. Linatimiza yale ambayo Bwana aliniambia katika mwaka wa 1933, mnaona, nasi tunasimama wakati huo asubuhi ya leo.

Naye Yesu Kristo, Neno, anahukumiwa, leo, kama ilivyokuwa kwenye kule kusulubishwa, na sasa yuko mikononi mwetu. Yeye yuko mikononi mwa ulimwengu. Neno limetambulishwa kwa dhahiri, kila mahali ulimwenguni, mnaona, Naye anasimama ndani akihukumiwa. Madhehebu yote yalimkataa. Na sasa Yeye anahukumiwa kama . . . katika Baraza la Makanisa, nao wanamkataa tena na kwa namna fulani wanachagua kama walivyofanya wakati huo.

83 Mnaona, maumbile katika historia hujirudia yenyewe, kwa maana maumbile huendelea vile vile yalivyo. Miti ingali

inaendelea kukua, na mboga zinachipuka, na maua, na ulimwengu unazunguka kama tu vile uzungukavyo daima. Ni maumbile. Na maumbile ya kila kipindi hutoa, tena, na kutoa tena m-mn'gao wa kile—kile—kile maumbile yalichokuwa hapo kabla yao. Na, leo, tunajikuta wenyewe tena tumesimama mahali pale pale.

Naam, Yesu alikuwa ni "Neno," Mtakatifu Yohana, sura ya 1. Sote tunaamini jambo Hilo. Yeye alikuwa Neno. Na kwa kuwa alikuwa Neno . . . Tafadhalini fahamuni. Yeye alikuwa ni Neno, Naye ilimbidi ayapinge yale madhehebu.

Nao hawaku-—wao hawakumkataa Yeye kwa sababu ya miujiza Yake. Hawakumkataa. Wao walisema . . . Yeye alisema, "Ni nani anayeweza kunishtaki Mimi?"

"Naye alikuwa amefanya uovu gani?" kasema maskini yule bibi. "Yeye amefanya uovu gani ila kuwaponya wagonjwa?"

84 Kasema, "Sisi hatumhukumu kwa ajili ya mambo haya." Mnaona? "Tunamhukumu Yeye kwa sababu Yeye, akiwa mwanadamu, anajifanya Mwenyewe Mungu." Na Maandiko yao wenyewe yalisema ya kwamba Yeye angekuwa Mungu.

Katika Isaya, yule nabii mashuhuri aliyeandika Vitabu sitini na sita vya Isaya, naye anaanza na . . . Mwanzoni, kama vile mwanzo; na katikati ya hicho Kitabu anatokea Yohana Mbatizaji; na kinaishia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Na vitabu sitini na sita katika Biblia, kama vile kulivyo na sura sitini na sita katika Isaya. Ni jambo la ajabu kwamba ndivyo ilivyo. Hii Isaya 9:6, yeye alisema, "Maana kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume; Naye ataitwa Jina Lake, 'Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye Nguvu, Baba wa milele, wa Ajabu.'"

85 Nayo mapokeo yenye upofu, ama taratibu, zisingeona ya kwamba huyo alikuwa Mungu; kwa nabii wao wenyewe, yule ambaye alijiliwa na Neno, yule aliyesema ya kwamba angekuwa ni Mungu. Taratibu zilizopofuka! Kwa hiyo wao walikuwa wamelikataa Neno, na kumtaka muuaji badala yake, Baraba.

86 Basi, leo, Neno, likiwa ni dhahiri kwa ajili ya siku hii, limethibitishwa. Limefanywa halisi. Limeonyeshwa kuwa ni Kweli. "Na katika siku za mwisho," kama alivyosema Yesu, "kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," na kadhalika, "ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Mungu yeye yule, Mwenyewe, Ambaye alikuwa ni Neno, alibashiri wakati wa mwisho, na ambayo yangetukia; na Nuru zingeonekana katika wakati wa jioni; na jinsi ambavyo, Malaki 4, Yeye angeyatuma mambo haya na kuyathibitisha.

87 Na jambo hilo limefikishwa mahali pa uamuzi, nayo makanisa yamelikataa. Basi makanisa yametaka nini? Muuaji wa Neno, mmoja anayechukua taratibu fulani. Kama hiyo taratibu inapingana na Neno, basi ni muuaji wa Neno. Nao

wametaka mapokeo ya kimadhehebu, badala ya Neno la kweli likidhihirishwa na kuthibitishwa kwamba ni Mungu kati ya watu; kwa sayansi, kwa picha, Nuru, Malaika yule yule wa Bwana, ile Nguzo ya Moto.

Yeye yule aliyeishi duniani katika—katika mwili wa Yesu Kristo, amekuja juu ya watu Wake katika siku za mwisho, ambapo sayansi imempiga Yeye picha. Kanisa limeona kazi Zake. Imethibitishwa kwelikweli, kwa kanda na kila kitu, kila mahali ulimwenguni tena na tena, na ikiwa imehudumu yenyewe.

Na hata hivyo, katika hayo yote, taratibu zao zinataka Baraza la Makanisa kuihukumu ile Kweli. Mnaona? Wanataka muuaji ambaye angefunga, ama kukomesha, ama kufunga. Na, litafanya hivyo, wao watakomesha Kitu kama hicho. Na italibidi Baraza la Makanisa kufanya jambo hilo. Hiyo hapo alama ya mnyama; dhidi ya Neno, ambalo ni Kristo. Bali si nini hii zao . . .

88 Wao wanafikiri ni mapokeo. Wao wanafikiri ya kwamba mapokeo yao ni ya Mungu. Mnaona? Bali hayatalistahimili Neno, wala Mungu hayathibitishi kuwa ni ya kweli. Yesu alisimama na Neno, lakini si na lile baraza lao; bali na Neno. Nalo Neno lilithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Mungu.

Nalo linathibitisha leo ya kwamba ni Mungu, kwa maana linaishi Maisha yale yale, linafanya jambo lile lile kati yetu lililofanya kule nyuma, na kubashiriwa.

89 Kwa hiyo wao wanafanya nini? Wanakubali kitu ambacho . . . Wao wamekubali, tayari, shirika lile lile litakalosulubisha Hilo. Na kusulubishwa kwa wasio wa madhehebu kumewadia. Hiyo ni kweli.

90 Naam, jambo hilo halipingi Maandiko. Linaambatana na Maandiko. "Nao wakafanya sanamu ya mnyama." Wakiunganisha madhehebu ya ulimwengu katika Protestanti moja, wakiunda ile alama ya mnyama, sanamu ya mnyama, kulingana na Ufunuo 13:8. "Nao wakafanya sanamu ya mnyama."

Yule *mnyama* ni "Rumi." Sote tunajua jambo hilo. Lakini daima imekuwa Rumi, yote . . . Inawezaje kuwa—inawezaje kuwa ni Urusi, wakati Biblia inasema ni Rumi? Mnaona, watu wanapata tu dhana mbaya. Mnaona? Inawezaje kuwa jambo lingine, wakati imetabiriwa kwamba haina budi kutoka Rumi?

91 Rudini kwenye Danieli tena, kile chuma na udongo miguuni; kile chuma hakikukoma, tangu magotini hadi mwisho. Na mtu ye yote anajua ya kwamba Urusi haikuwa hata inajulikana wakati huo. Ilikuwa ni Rumi. Lile joka jekundu lilikuwa ni Rumi. Daima ni Rumi. Nacho hicho chuma hakikubadilika kamwe kuwa kitu kingine, kutoka Rumi hadi kitu kingine; kilibakia Rumi. Naye yule mnyama ni Rumi!

92 Nayo Rumi ilikuwa na utaratibu wa kidini ambao kichwa chake cha kufisha . . . ama jeraha la kufisha lilimuua kichwani mwake, bali alifufuka tena, kutoka Rumi ya kipagani hadi Rumi ya kipapa. Nao sasa watafanya sanamu yake, kutokana na mnyama anayetoka Ufunuo 13.

Hivi mliwahi kuona? Taifa hili ni namba kumi na tatu, na linaonekana . . . Sisemi jambo hili ndilo . . . Ni—ni ajabu, hata hivyo, kwamba lingetukia kihesabu, he- . . . likiambatana vizuri kabisa na Maandiko. Linapatikana katika sura ya 13 ya Ufunuo, taifa hili.

93 Wanyama wale wengine wote walitoka majini, ambayo ni umati na wingi wa watu, Biblia ilisema; bali mnyama huyu mdogo alitokea nchini, mahali pasipokuwa na watu. Hata hivyo, yeye alikuwa ni mwana-kondoo, uhuru wa dini; kisha akanena kama joka, na kujiunganisha mwenyewe na mamlaka na kufanya yale yote yule joka aliyofanya kabla yake. Sawa kabisa. Kwa hiyo haya basi. Ha—haina budi kuwa namna hiyo. Hakuna njia nyingine ya kuliepuka.

94 Nasi tupo hapa, leo, tukiunda shirika. Madhehebu! Hatuwezi kungojea hata baadhi . . . Tulijaribu kumfanya kila mmoja kuwa M—Mluteri; wala hatukuweza kufanya jambo hilo. Kujaribu kuwafanya wote wawe Batisti; hatukuweza kulifanya. Wote wawe Methodisti, ama wote wawe Pentekoste; hawakuweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, ili kufanya jambo hili, wakati ni mfupi sana, wao wameunda halmashauri, kichwa, sanamu ya mnyama. Hivyo ndivyo wamefanya hasa. Na ni kitu gani? Kusulubishwa kwa Neno, tena, kumewadia. Liko hukumuni na karibuni litafika ukumbini.

95 Angalia, Neno lililodhihirishwa, kutoka kwenye madhehebu. Linadhihirisha. Ne—Neno ni tofauti na madhehebu.

Hii ni nini, shirika hili ni nini? Ni kibaraka wa Rumi. Je! Biblia ilisema itakuwa hivyo? Naam, bwana! Ufunuo 17, wao waliona Rumi ikijiinua yenyewe katika shirika la kidini, la mwanamke. Mwanamke, kanisa daima linawakilishwa na mwanamke.

Maana, Bibi-Arusi wa Kristo ni mwanamke. Hawa ndiye aliyeanguka; Ndiye atakayekombolewa. Nalo Kanisa (ni kitu gani?) ni mwanamke anayekombolewa.

96 Na mwanamke huyu aliketi juu ya mnyama mwenye vichwa saba. Nasi tunajua juu ya hivyo vilima saba, na kadhalika, kama Biblia ilivyosema ingekuwa. Hakuna kosa. Hakuna nafasi ya kosa. Mnaona?

Ndipo angalia basi, tunaona, ya kwamba yeye alikuwa "MAMA WA MAKAHABA." Mnaona? Basi mama na binti wanaungana pamoja tena katika urafiki. Ambapo, wakati mmoja, huyo binti alimtoroka mamaye, kujaribu kuishi

kistahifu, kwa maana mamaye alikuwa duni sana na mtovu wa uadilifu hata huyo msichana akaondoka nyumbani. A-ha. Lakini sasa, kwa kuwa ameanza kupevuka kidogo, yeye, na kufanya mambo mengi sana maovu, yeye mwenyewe; anamwona mamaye, anafikiria mamaye alikuwa sahihi, kwa hiyo yeye anaunda shirika la kwake. Mnaona? Barabara.

97 Kuunganisha umadhehebu, Uprotestanti, kunatimiza sawasawa Maandiko yalivyosema katika Ufunuo 17. "Wote, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, walikuwa wake." Mmoja ama mwingine, aidha yule mnyama au ile sanamu ya mnyama. Biblia ilisema jambo hilo.

Naye Yesu alinena juu ya jambo hili, si kama ukomunisti. Lakini katika Mathayo sura ya 24, kuanzia aya ya 21 hadi ya 26, Yeye alibashiri ya kwamba roho hiyo katika shirika hili ingefanana sana na kitu kilicho halisi hata ingewadanganya walio Wateule kama yamkini; walio Wateule, ambao majina yao yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na, kweli, imewafunga sana, hata akasema kama asingefupisha ile kazi, kwa ajili yao, kusingekuwa na mwenye mwili ye yote angaliokolewa juu ya nchi. Nasi tuna nini hii tu . . .

98 Huu ni—huu ni '64, sivyo? Nami nafikiri wao wanadai yapata miaka kumi na saba imetolewa humo, hivyo, kulingana na kalenda. Nasi tuna '64, 1964, ambalo litafanya (ni kitu gani hicho) miaka thelathini na sita iliyosalia, kufikia karne ya ishirini na moja.

Na kila baada ya miaka elfu mbili, ulimwengu umefikia mwisho wa taratibu zake, taratibu za dini, kwenye mwisho wa taratibu zote, na Mungu ilibidi kuingilia kati. Alifanya hivyo katika siku za Nuhu; miaka elfu mbili ya kwanza. Miaka elfu mbili ya pili; huo utaratibu umerudia mahali ambapo fungu letu la maneno linasimamia, asubuhi ya leo, ndipo Yeye akatuma tena Neno Lake. Yeye akatuma Neno Lake kwa nabii, wakati wa Nuhu, nabii Nuhu; nao watu wakalikataa, kwa ajili ya shirika lao. Alituma Neno Lake tena katika siku za Yesu, Neno lililodhihirishwa katika ukamilifu; watu wakalikataa. Na sasa ni mwaka wa 1964, ikiacha miaka thelathini na sita kufikia miaka elfu mbili zaidi; nalo Neno limetolewa, nalo shirika limelikataa.

99 Tuko karibu kiasi gani? Huenda ikawa muda umeendelea sana kuliko tunavyodhania, mnaona, kwamba wakati wo wote ingeweza kutukia. Labda imetendeka tayari, tujuavyo sisi, kama nilivyonena Jumapili ya mwisho niliyokuwa hapa. Huenda jina la mwisho likawa lilikuwa kwenye Kitabu hicho; litakapokuwa mle, hakuna wakati mwingine wa kuingia. Ulimwengu utaendelea tu kama ulivyokuwa, bali Kanisa

limetiwa muhuri. Angalieni sasa tunapoendelea hapa. Majina yao, sasa, hatawapoteza hao ambao majina yao yameandikwa.

100 Ni kitu gani? Haina budi kuwa ni shirika fulani. Mnaona? Basi wazia tu, kuwa mfuasi wa madhehebu hayo katika shirika hilo, unafanya nini basi? Umefanya wapi? Umefungiwa nje, unaona, kutoka kwenye Neno, ukaingizwa kwenye shirika la kuua linaloondoa, "La kuwa na mfano wa utauwa, bali likikana Nguvu zake." Ni alama ya mnyama. Kabisa. Mnaona?

101 Ni mnyama aliye kule, yale aliyofanya; na hii hapa ile sanamu, jambo lile lile. Na yule mnyama alikuwa mkubwa sana, aliyeunda lile kanisa la ulimwengu mzima kule Nikea, mnaona, hata wao wakafanya nini hii yote—ulimwengu mzima kuja kwenye hilo, kwenye shirika hilo moja. Nao walifikiri ni kuu mno, "Hakuna aliyeweza kufanya vita nao," Biblia ilisema, hata wakafanya sanamu ya yule mnyama, na kuwaleta Waprotestanti wote katika Baraza la Makanisa; ambayo yaliunda shirika, hata hukufikiriwa kama Mkristo wala cho chote kile isipokuwa wewe ni mfuasi wa shirika hilo.

102 Hiyo ndiyo tofauti kati ya alama ya mnyama na kutiwa Muhuri wa Mungu. Mungu hutia muhuri kwa Neno Lake. Mnaamini Neno ndilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Sasa mnasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?" Naam, bwana.

103 Naam, najua ninyi Wasabato, ama Waseventh-day Adventistists, mnasema, "Kushika siku ya Sabato." Lakini hiyo siyo. Si kuwa mbaya kwenu, lakini hilo si la kimaandiko kabisa.

Waefeso 4:30, inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Mnaona?

104 Naam, Roho Mtakatifu ni Neno. Mungu si watatu. Yeye ni Mungu yeye yule katika nyakati tatu, afisi tatu. Mungu, Baba, juu ya torati; Mungu, Mwana, katika neema; na Mungu, Roho Mtakatifu, kama mnavyomwita Yeye, Mungu yule yule katika wakati wa Roho Mtakatifu. Mungu, Baba, alikuwa ni Neno; Mungu, Mwana, alikuwa ni Neno; na Mungu, Roho Mtakatifu, ni Neno. Mnaona, ni afisi tatu tu. Na, pia, sisi . . . Naye Roho Mtakatifu hukutia muhuri, kwa hiyo wewe umetiwa muhuri kwa Neno.

Sasa unasema, "Vema, mimi nimetiwa muhuri na . . . "

105 Vema, basi, linajitambulisha lenyewe. Mnaona? Linathibitisha. Huwezi kuwa mfuasi wa shirika fulani, na uwe umetiwa muhuri kwa hilo shirika pamoja na Neno, mnaona, maana zinapingana, moja kwa jingine. Huwezi kufanya jambo hilo. Vema.

Sasa tunaona, ya kwamba, mitambo ya ile mashine kubwa, ile mitambo ya ile mashine kubwa, ambayo ita- . . .

Mashine, una . . . motokaa, ina pistoni, valvu, na kabureta, na kadhalika. Hiyo ndiyo—hiyo ndiyo mitambo ya kuendeshea.

106 Ningetaka kusema jambo fulani kwa Kanisa papa hapa, linanikumbusha. Mnaona, hilo ndilo . . . Ninaamini tumekaribia mwisho mno, ni—nitasema jambo fulani sasa. Mnaona? Mnaona? Ile—ile mitambo, kuna watu wengi sana wanaojaribu kuelezea ile mitambo wala hamuijui. Mnaona? Jambo pekee wewe . . . Na, mwajua, mnapaswa kujua jambo hilo. Mitambo inajulikana. Sasa vipi kama Musa . . .

Vipi kama mtu fulani angalisema, "Nuhu, ninataka uelezee jinsi ile—ile vile safina inavyoelea. Inatendekaje?" Asingeweza kufanya jambo hilo.

Si lazima ujue ile mitambo; ni Nguvu Zake tu za Utendaji. Mnaona, Nguvu za Kuendesha ndizo mnazotaka kujua.

"Vipi?" Vema, kama mtu fulani alikuja kwa Israeli, na kusema, "Aisee, Musa, nataka kufahamu. Uliwezaje kuumba wanyama kwa neno lako mwenyewe?"

107 Akasema, kasema, "Si neno langu. Ni Neno la Mungu. Yeye aliniambia nifanye jambo hilo." Mnaona?

108 "Mi—mimi—mimi . . . Niambie, nieleze jinsi ulivyowafanya nzi waje juu ya nchi, wakati hakukuweko na ye yote, nzi wengi jinsi hiyo juu ya nchi." Mnaona? Musa asingeweza kueleza jambo hilo, yeye mwenyewe. Haikubidi kufanya hivyo. "Ungeufanyaje upepo wa mashariki uje utoboe shimo kutoka upande mmoja hadi mwingine wa Bahari ya Shamu, nasi sote tukakufuata kwenye nchi kavu. Eleza namna ya kufanya jambo hilo. U—u—ulitumia ka—kanuni gani, Musa? Ipi? Niambie utafiti wa sayansi kwamba ni atomi gani uliyoachilia." Mnaona? Mnaona?

109 Yeye hakujua. Yeye, vema, hakujua ile mitambo; yeye alijua tu zile nguvu za utendaji. Na—na hiyo ndiyo njia.

Siwezi kuwaambia jinsi ninavyoishi. Siwezi kukwambia jinsi unavyoishi, bali unaishi. Siwezi kukwambia jinsi moyo wako, na chakula chako kinavyoingia na kutengeneza damu. Na kuchukua ngu—nguvu za hicho chakula, ki—kisha kinaenda kwenye ukuta wa tatu wa kinjia cha utumbo mdogo na kukigeuza tena kuwa uhai wa damu, na kuirudisha ndani yako. Si—siwezi kueleza jambo hilo, bali kinafanya jambo hilo. Mnaona, kinafanya jambo hilo. Si—siwezi kulieleza. Mimi siijui hiyo mitambo. Ni nguvu za utendaji.

110 Naam, Musa huenda ikawa alikuwa amejua ile mitambo, bali haikuwa kazi ya mtu mwingine kuifahamu ila Musa. Wao walijua ilitenda kazi, na hilo huridhisha. Mbona watu wasiridhike namna hiyo leo? Mnaona? Kila mtu asingeweza kuwa Musa. Kulikuweko na Musa mmoja tu. Wao walijua tu lilikuwa ni jambo la Mungu. Waliona jambo hilo lilikuwa ni la Mungu.

Nao wakafuata na kufanya vizuri mpaka walipoanza kulihoji hilo, walitaka kumwinua mtu mwingine kufanya jambo lile lile, Kora, Dathani. Nao walipompata mtu wa kuingiza maigizo ya kimwili, hatimaye Mungu alisema, "Jitenge. Usiingie kwenye huo utaratibu wa kimadhehebu. Mnaona, tokeni humo! Nitaumeza." Ndipo akaifungua nchi na kuumeza. Mnaona?

111 Hujui, si lazima uijue ile mitambo. Jua tu zile nguvu za kuendesha, kile kitu kinachoifanya itutume, kinachoifanya kuwa kweli, kisha uone kama litaelekea kwenye lengo ambalo Biblia iliahidi italifikia katika siku hii. Mnaona, ni Neno tena, kurudi kwenye Neno.

112 Sasa, mashine kubwa inawekwa sasa, na iko tayari kufanya kazi. Mitambo tayari iko pale. Wao tayari wana utaratibu wa kimitambo wa madhehebu ambao utaleta, juu ya nchi, "amani fulani," wao wanasema. Wao wana-. . . kama U.M.

Mataifa yameungana pamoja. Ni wakati wa kuungana. Hivi punde nilihubiri jambo hilo, juzijuzi. Wa. . . Wao wanaungana pamoja, kuleta kitu gani? Amani ya ulimwengu. Wao walifanya hivyo katika lile Shirika la Mataifa. Wamefanya hivyo daima, na haifanikiwi. Haiwezi kufanikiwa kamwe. U.M. si kitu ila baluni kubwa la mpira linalochukuliwa huku na huko na upepo wa mafundisho ya kila taifa. Litapasuka na kulipuka kwa kitu cho chote. Hauwezi kufanikiwa.

Wala Baraza la Makanisa haliwezi kufanikiwa. Ni shirika la mwanadamu, lisiloambatana na utaratibu. . . ama pamoja na utaratibu wao unaopingana na Neno la Mungu, na jambo hilo haliwezi kufanikiwa. "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" Huwezi kufanya jambo hilo. Na kanisa la Kikristo lawezaje, litapaswa ku-. . .

113 Wa—Wapentekoste, Waassemblies of God, na—na makanisa mengine makubwa ya—ya milki ya Kipentekoste, na ya watu wa Injili Yote, wanawezaje kuacha mafundisho yao ya kiinjilisti, kanuni zile zile ambazo wamezisimamia? Na mahali walipolelewa, kutoka kwenye madhehebu hayo na kuyalaani; nao hawana budi kuacha fundisho lao la kiinjilisti, kutembea na mtu wasiokubaliana naye juu ya kanuni za Biblia, na Kuponya Kiungu, na Nguvu za Mungu, na Yesu Kristo. "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?"

114 Haya basi, hiyo ndiyo saa tuliyofikia, na hiyo ndiyo ile mashine kubwa ambayo imewekwa. Sasa wao wana mitambo. Kitu tu wanachopaswa kuwa nacho ni Shetani aingie ndani mle, pamoja na zile nguvu za utendaji, kushurutisha kutiwa alama ya mnyama. Wakati kutakapolazimishwa, basi nguvu za utendaji zinafanya kazi. Mitambo ipo. Wanayo tayari.

115 Hebu niseme jambo fulani, pia; wakati huu wa kuungana, kuona makanisa yakiungana, mataifa yakiungana. Ni wakati wa kuungana kwa Mungu na Bibi-arusi Wake, pia. Nami nasema

jambo hili kwa kicho na heshima. Ninaamini Bibi-arusi wa Kristo ameitwa. Ninaamini ametiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Ninaamini mitambo ipo. Wanangojea Nguvu za Utendaji zitakazomwondoa duniani, kuingia Utukufuni, katika Kunyakuliwa. Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote. Naam, bwana. Hatujui jinsi Yeye atakavyofanya jambo hilo, bali atalifanya.

Yeye ndiye Nguvu za Utendaji. Sisi tunafanyika tu washiriki wa hiyo mashine, ya Mwili Wake, tukijifanya wenyewe kuwa katika sura Yake, na kumwona Yeye akijiunganisha nasi, katika kazi Zake, pamoja na karama Zake za upendo, huku akitupa sisi hizo kabla tu ya ile Karamu ya Arusi. Nasi tunangoja, tukitazamia jambo hilo.

Kanisa lao kubwa, pia, linaunganishwa.

116 Nguvu za Utendaji za Kanisa hili zitakuwa kujazwa tena kwa Roho Mtakatifu ambaye tumetenda kazi naye kwa kiasi kidogo wakati lile Jiwe la Kufunika linashuka kuungana na ule Mwili. Lakini wakati Kichwa hicho na Mwili huo vitakapoungana pamoja, zile nguvu kamili za Roho Mtakatifu zingemwinua juu barabara namna hiyo; hata waliokufa, waliokufa katika Kristo, kwa mamia ya miaka iliyopita, watainuka katika uzuri wa utakatifu Wake, na kuruka kwenda hewani. Zile Nguvu za Utendaji ni Roho Mtakatifu.

117 Na sasa nguvu za utendaji za shirika hili kuu walilounda, mashine hii kuu itatenda kazi siku moja katika Baraza la Makanisa yaliyoungana Ulimwenguni, ambalo litalazimisha, pia. Kumbuke-. . . lakini kumbukeni . . .

Unasema, "Wakati jambo hilo litakapotendeka . . ." Utakuwa umechelewa sana wakati huo. Wewe tayari uko ndani yake. Ama unataka kuwa, ama hutaki, uko kule tayari. Unaona? Angalia, tayari una roho huyo juu yako.

118 Katika siku ambayo—ambapo pe—pepo za Roho zinavuma kutoka mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini, zikiwashawishi watu kutoka kwenye kitu hicho, na kuwaonyesha watu!

Hiyo ndiyo sababu nimekuwa nikipinga sana utaratibu huo. Niliona kulikuweko na kitu fulani humo, giza fulani. Kama nilivyowaona wanawake hao jinsi walivyojitia vitu hivyo usoni mwao, niliwaambia Jumapili iliyopita, nilijua kulikuwa na kitu fulani kinakuja.

119 Ni kwa nini mimi daima nilipinga kitu kama hicho? Sikujua jambo hilo; sasa najua. Kwa nini daima nilipinga madhehebu ya dini? Ni kwa sababu (naliona jambo hilo sasa) ni ile alama ya mnyama. Mnaona? Sikusema jambo hilo hata kwenye majuma machache tu yaliyopita. Mnaona?

Naam, baada ya siasa za kanisa, kitu gani basi kinatukia? Baada ya Neno kuthibitishwa kweli? Naam, angalia, hatimaye imefikia mahali hapana budi kuwe na mapatano. Hatua yao inayofuatia sasa ilikuwa . . .

120 Hatua ya pili ya Wayahudi ilikuwa ni nini baada ya kanisa kulikataa? Kanisa lililikataa Neno. Hawakutaka uhusiano wo wote Nalo. "Ilikuwa ni pepo mchafu." Lilijua mawazo yaliyokuwa katika moyo wao. "Lilikuwa chafu." Hata hivyo, ilikuwa ni Neno. Kazi alizofanya, zilimshuhudia Yeye, zikathibitisha Yeye alikuwa ni Nani. Wao hawakutaka uhusiano wo wote Nalo.

Ndipo, jambo lililofuata, linafikia kwenye serikali. Na hii ni serikali ya kanisa, kwa maana taifa zima linahusika. Kulikuweko na taifa la kipagani likilitawala taifa la kidini. Naam, ni, jambo lote ni dini, kwa hiyo haina budi kufikia kwenye dini ya ulimwengu.

Loo, jamani, kipofu angeweza kuona jambo hilo! Basi kipofu anasema nini anapoona jambo hili? Anapoliona, atatoka kwenye upofu wake.

121 Angalia pale wakati baraza hili la ulimwenguni linapokutana, "Tutamtendaje huyu Yesu aitwaye Kristo?" Bila shaka hawataki uhusiano wo wote Nalo. Kwa hiyo kuna jambo moja tu la kufanya, basi, ni vile kabisa walivyofanya wakati huo, watalisulubisha, bila shaka, watalinyamazisha. "Haliwezi kuweko tena. Halitaruhusiwa kufanya jambo hilo." Nguvu za dini za mataifa hazitawaruhusu kufanya jambo hilo tena. Huduma kama hii inayoendelea hapa, na mambo kama hayo, yatafungwa kabisa. Huwezi kutenda kazi bila kibali kutoka kwenye makao makuu, kichwa cha kanisa, mnaona, sanamu ya mnyama. Loo! Tumewasili, hivyo tu. Tume—tume—tumewasili.

Na kuthibitishwa kweli; hatua ya pili ni kumsulubisha.

122 Ni kama ilivyo sasa, kuwafanya wote wasiojiunga nao, watafungiwa nje wala hawataruhusiwa kuhubiri, mnaona. Hilo linalisulubisha, upya, Neno lililothibitishwa la ahadi. Linalinyamazisha, "Hamruhusiwi kuwa nalo tena. Hakuna tena ibada za kuponya. Hakuna tena kuwaombea wagonjwa. La, bwana! Huwezi kufanya jambo hilo. La, hakuna mengine ya haya. La, bwana! Mtapitia katika Baraza la Makanisa la sivyo hamna kitu hicho kabisa."

123 Sasa mnaweza kuona ni kwa nini ninapinga madhehebu ya dini, kwa sababu ni alama ya mnyama. Rumi ndiyo kichwa chake, cha kwanza. Hilo ni sawa kabisa. Naye anawafanya wote waichukue kwa kujiunga na wale binti, hiyo ndiyo ile sanamu. Mama yake alifanya kitu kile kile. Rumi ilifanywa madhehebu wapi kwanza? Dini ya kwanza kuunda madhehebu duniani ilikuwa ipi? Katoliki ya Kirumi. Mtu ye yote aliye na neno linalosema sivyo ilivyo, hebu nilisikie tu. Halipo hapa.

Madhehebu ya kwanza, kanisa la kwanza lililopata kufanywa madhehebu, ilikuwa ni kule Nikea, Rumi. Naam, bwana. Na hivyo ndiyo walivyofanya hasa.

124 Naye Luther alifanya nini baada ya kifo chake? Walifanya jambo lile lile walilofanya huko Nikea, Rumi. Walifanya nini baada ya Wesley? Walifanya nini baada ya ile mienendo yote mikuu iliyozuka? Walifanya jambo lile lile, wakafanya binti za yule kahaba, kikamilifu tu hasa. Kama, kwa jambo lile lile, tunaona hapa . . .

125 Nilikuwa na Andiko dogo lililoandikwa hapa. Labda afadhali niliache hilo. Lakini, basi angalieni, wao walikuwa . . .

Madhehebu ya kanisa yana taratibu ile ile leo. Kitu tu wanachohitaji ni nguvu zake za utendaji, kitu tu cha kukianzisha. Nayo yanafikia kwenye shindano la kuamua, mara moja.

126 Kanisa Katoliki na makanisa ya Kiprotestanti yatakuwa rafiki. Nimewaambia jambo hilo tangu—tangu zamani, kwa miaka thelathini na kitu iliyopita. Wao wataungana pamoja. Nanyi mnaona kile hasa wanachofanya sasa. Mpro—Mprotestanti kamwe hatakuwa Mkatoliki, bali watakuwa shirika la kindugu, alama ya mnyama, iliyofanana na yule mnyama.

127 Kama kwa njia ile ile ambayo yule mama, Hawa, alivyouchafua ulimwengu mzima kwa mauti ya kimwili. Yule mama, Hawa! Sikilizeni. Mama Hawa aliiharibu jamii nzima ya kibinadamu, kwa mauti ya kimwili, (vipi?) kwa kulikataa Neno na kukubali kitu kilichofanana sana Nalo. Yeye alisababisha mauti yote ya kimwili kwa maana aliliacha Neno la kweli, na kuamini Neno la kweli lote ila kidogo tu. Kutokukubaliana kumoja kudogo na Neno kamili la Mungu kulisababisha kila kuumwa na moyo, kila mauti na kila kitu kilichowahi kuwa duniani. Hawa alifanya jambo hilo, mama wa mauti. Sasa mnaona mahali tunapokuja? Mama wa mauti, angalieni, yeye alikosa tu kuliamini Neno.

Alisema, "Mungu amesema . . . "

Shetani akasema, "Hiyo ni kweli."

"Mungu amesema . . . "

"Hiyo ni kweli."

"Mungu amesema . . . "

"Hiyo ni kweli."

"Mungu amesema . . . "

128 "Naam, hilo, sawa. Kwa—kwa namna fulani, hilo ni sawa, lakini, unaona, hayo—hayo—hayo si Yote. Unaona, ma—macho yako yatafunguliwa, utakuwa . . . "

Lakini Mungu amesema, na hilo latosha, Neno! [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.] Mnaona, ilianza na kuelewa vibaya kudogo tu kwa Neno, na, jambo lile lile, inaishia vile vile.

129 Angalia, binti ni mzao wa mama na baba, kwa kuungana. Sasa hapa pana jambo la kushangaza. Lakini mauti, ya kimwili, mauti ya kimwili ni kuungana kwa mama Hawa na Shetani, pamoja, kwa kutokuamini Neno la Mungu. Wao waliungana na kuleta ma—matokeo ya kifo. Yeye, yale. . . Mauti ni matokeo ya kuungana kwa Shetani na Hawa, pamoja.

130 Hawa alikuwa na Neno. Shetani analipinga Neno. Basi, angalia, karibu tisini na tisa na tisini na tisa juu ya mia Yake, Shetani alikubali ilikuwa ni kweli. "Zitafanana sana," Biblia ilisema, "katika siku za mwisho, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Mnaona jinsi linavyokuja, jinsi imekuwa daima, jinsi linavyomalizika? Jinsi ile ile, kuungana kwa kutokuamini katika Neno lote la Mungu. Mmelifahamu? Huko ndiko kulikoleta kifo, ni kuunganisha kutokuamini na Neno. Kutokuamini, kidogo tu, sehemu ndogo sana yake; ndogo, ndogo sana, ndogo mno, moja kwa mia ya asilimia moja. Lakini halina budi kuwa asilimia mia moja! Hivyo tu.

131 Angalieni, binti ya Mungu, Kanisa, Bibi-arusi, pia ni mzao, wa Mungu na Neno Lake, wakiungana. Roho Mtakatifu akiunganika katika mwili wa nyama, Yeye alimzaa Mwana wa Mungu, mzao wa haki ya Mungu. Na katika siku ya mwisho, kama tunavyoambiwa, "kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," Bibi-arusi ataunganishwa na Neno la Mungu lililodhihirishwa katika mwili, Roho Mtakatifu akiwatia muhuri katika Mungu, na kutia muhuri kutokuamini nje, upande wa nje.

132 Kama nilivyosema, kama uhai wa Beethoven ulikuwa ndani yako, ungeishi kama Beethoven; kama uhai wa Hitler ungalikuwa ndani yako, ungeishi kama Hitler. Na Uzima wa Kristo ukiwa ndani yako, utaishi kama Kristo, na kazi za Kristo utazifanya. Hilo litatendeka. Kama Kristo angaliishi leo, Yeye angefanya kile hasa Neno lilichosema angefanya leo. Na kama Neno lilisema kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," kwa nini ulimwengu huu wa dini uliopofuka usione wakati wanaoishi? Mnaona?

133 Hawa alisababisha mauti yote ya kimwili, kwa kujaribu kuingiza uzushi fulani wa Shetani katika Neno. Na hilo ndilo jambo lile lile lililotukia kwa kanisa, kule Nikea, Rumi, kwa kuchukua mafundisho ya sharti badala ya Neno. Hilo ndilo jambo lile lile katika Methodisti, Batisti, Presbiteri, wakati Nuru inapojitokeza katika kila wakati nao wanaikataa.

Hiyo ndiyo sababu Mluteri alikufa wakati Wesley alipoinuka. Ilikuwa ni wakati mwingine. Neno lilikuja, nao iliwabidi walikubali la sivyo wafe. Hiyo ndiyo sababu

Wapentekoste wanakufa sasa, kwa sababu ule wakati umewadia. Neno limedhihirishwa, wakati wa tai, wakati wa Neno kurudi, "kuirudisha Imani ya baba, iwarudie watoto tena." Nao wameungana sana, wanalikataa, nao si kitu ila mauti ya kiroho. Daima . . .

134 Mwili wa Mungu, ulioungana kama Bibi-arusi Wake, ukiwa Mmoja; Yeye na Kristo, pamoja, ni Roho akitenda kazi katika mwili wa Kanisa kama alivyotenda katika mwili wa Yesu Kristo, maana ni sehemu ya Mwili Wake. Si wawili; bali Mmoja! Wao ni Mmoja. Mume na mke si wawili tena, bali ni mmoja. Naye Kristo na Mwili Wake ni Mmoja. Na Roho yule yule aliyekuwa katika Kristo yuko katika Bibi-arusi Wake, katika Mwili Wake, ambaye huwaunganisha pamoja na Neno lote. Naye Mungu akiishi mle, Yeye Mwenyewe, akidhihirisha jambo hilo.

135 Naye mpinga Kristo, atasema, "Loo, ninamwamini Kristo, ninaiamini Injili, ninaamini Mambo haya, lakini, wajua . . ." Haya basi. "Lakini, unajua, siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho, mnaona." Haya basi. "Loo, siamini inakubidi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo."

136 Bali Biblia ilisema ilikubidi. Sasa nataka mwanatheolojia fulani akanushe jambo hilo. Mnaona? Mnaona? Halina budi kuwa hivyo. Mnasema, "Vema, ubatizo hauleti tofauti yo yote." Vema, basi, kwa nini ukaandikwa? Kwa nini ukaleta tofauti kwa Paulo? Kwa nini ukaleta tofauti kwa wengine wote? Aidha wewe umebatizwa . . .

Biblia ilisema, "Una jina la kuwa hai, nawe umekufa," maana hakuna jina lingine walilopewa chini ya Mbingu.

Kwa nini uhubiri katika Hilo, uombe katika Hilo, na cho chote kile, lakini, unapofika kwenye kidimbwi, unalikataa? A-ha. Mnaona?

Nilimwambia mtu fulani juzijuzi, nikasema, "Vipi kama mtu . . ."

Akasema, "Haileti tofauti yo yote."

137 Nikasema, "Kama mtu akija kwako, halafu aseme alibatizwa katika jina la 'Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, na Nyota ya Asubuhi,' ungesema yeye ni sawa?"

Akasema, "La, bwana."

Nikasema, "Ungembatiza tena?"

"Naam."

Nasema, "Ungebatiza namna gani?"

Kasema, "Katika jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.'"

138 Nikasema, "Vema, sasa ulifanya vile hasa, uliweka . . . Kama unaviita hivyo 'majina,' ulifanya jambo lile lile alilofanya wakati aliposema, 'Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, na Nyota

ya Asubuhi,' kwa maana hicho ni cheo, na 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu' ni cheo. Unaona?"

Akasema, "Lakini Yesu alisema mkabatize, 'Jina.'"

139 Nikasema, "Hivyo ndivyo alivyomaanisha kufanya hasa. Bali katika, si—si . . . Yeye hakusema, 'taja maneno haya.' 'Wabatizeni katika Jina,' Jina! Loo, jamani!" Nikasema, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu' ni vyeo. 'Jina la Baba, Mwana. . . . Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.'" Mnaona?" Nikasema, "Petro alisema Hilo lilikuwa ni lipi? Hao wengine walisema lilikuwa ni lipi? Mnaona? Ni lipi? A-ha. 'Bwana Yesu Kristo' ndilo Jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.'" Yeye ana yapata wananchi elfu thelathini wanaokubidi kuwabatiza tena sasa. Mnaona? Vema. Lakini hilo ni kweli. Paulo alisema, "Kama Malaika akitoka Mbinguni . . . "

140 Paulo aliwaambia hao watu ambao hawakubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Matendo 19:5, kwamba, ili kumpokea Roho Mtakatifu, iliwapasa kuja. Ingawa walikuwa wakipiga makelele na kumsifu Mungu, na kufanya mambo makuu, yeye alisema iliwabidi kurudi na kubatizwa, tena, katika Jina la Yesu Kristo. Baada ya Yohana Mbatizaji kuwabatiza, iliwabidi kurudi na kubatizwa tena.

Naye alisema, katika Wagalatia 1:8, "Kama Malaika akitoka Mbinguni na kufundisha jambo lingine ila nililowafundisha, na alaaniwe." Naam, bwana. Kwa hiyo hatuna budi kudumu moja kwa moja na Neno hilo, kila Neno Lake. Mnaona?

141 Angalia. Loo, usiwe na waa lo lote; uwe na hakika kabisa. Kama kuna jambo lo lote linalotilia shaka moyoni mwako, afadhali ulirekebishe sasa. Usingoje hata wakati huo, muda umeenda sana. Usingoje hata utakapoichukua ile alama kindani sana hutaweza kuliona tena, utakuwa kipofu.

Yeye aliwapofusha Israeli, ili kwamba alidhihirishe Neno Lake. Yeye anafanya jambo lile lile kwa Mataifa, maana hapa—hapa wanaelekea moja kwa moja kwenye kitu hicho jinsi ile ile tu walivyofanya wakati ule.

142 Angalia, Hawa alikataa na kupoteza haki zake. Baada ya yeye kuona Neno limethibitishwa na Mungu, yale aliyokuwa amefanya, alilikataa na kupoteza haki zake. Jambo lile lile walilofanya kule Nikea, Rumi. Na wanafanya jambo lile lile sasa kwenye Baraza la Makanisa, vile vile hasa. Ndugu, hilo hapo, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, jambo lile lile. Hivyo ndivyo Israeli walivyofanya. Hivyo ndivyo alivyofanya Pilato. Hivyo ndivyo jambo lote linavyofanya, daima, tangu Hawa hata sasa, jambo lile lile. Wao hulikataa Neno lililothibitishwa na kuchukua fundisho la sharti, badala yake. Hilo husababisha mauti, mauti ya kiroho.

Wafu! Neno lingali linahubiriwa kwa wafu. Barabara! Haitakuwa katika ule Utawala ya Miaka Elfu, sasa, mnaona.

Wao—wao, wamekwisha kuhubiriwa. Labda wanalipata sasa hivi. Mnaona?

143 Wana wa Kaini, ambao walikuwa ni matokeo ya kutokuamini Neno la Mungu, wana wa Kaini waliudhihaki ujumbe wa nabii Nuhu. Mnaona jambo hilo? Kwa Neno la Mungu yeye alikuwa ameleta hu—hukumu iliyobashiriwa, naye alikuwa na ishara dhahiri, ishara zilizothibitishwa ya kwamba wakati ulikuwa umefikia mwisho, nao wana wa Kaini wakaudhihaki Huo.

Ndivyo wanavyofanya sasa. Kwa hiyo, hilo, walifanya jambo hilo katika siku za Yesu. Ndivyo walivyofanya katika nyakati zote. Imekuwa hivyo daima. Wanaudhihaki na kuufanyia mzaha. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho watakuweko wenye kudhihaki, wakisema, 'Hakuna tofauti katika majira, tangu baba zetu kulala mauti.'" Ninyi, mnaona?

144 Vivyo hivyo wana wa ibilisi, kupitia taratibu za dini, kwa Neno lililodhihirishwa katika wakati wa Yesu Kristo. Angalieni, taratibu za dini za Wayahudi, [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha, na kusema, "Dada Rose."—Mh.], Wayahudi ambao iliwabidi kujua vyema zaidi, lakini taratibu zao ziliwafanya kulikataa na kulidhihaki Neno la Mungu (ambalo wao walidai waliliamini) lililodhihirishwa, hakuna hata Neno moja lililoenda kando. Wao walifanya jambo lile lile.

145 Vile vile wanavyofanya leo. Taratibu ya dini katika mashine hii kubwa ambayo wameitayarisha sasa, itafanya hivyo, imezikataa katakata ahadi katika wakati wa mwisho; pamoja na Ujumbe wa wakati wa mwisho, na ishara ya wakati wa mwisho, kila kitu cha wakati wa mwisho kinachopaswa kuweko, kama Mungu alivyobashiri jambo hilo, Neno kwa Neno.

Liko kwenye kanda. Kama—kama wao wakinipiga risasi, ama lo lote wanaloweza kufanya, wao kamwe hawataunyamazisha Ujumbe huo! Mnaona? Utaendelea tu jinsi ile ile. Mnaona? Tayari umetoka. Umerekodiwa. Umetoka. Mnaona? Wasingeweza kamwe. . . Ni—Ni Neno la mwisho, sasa hivi. La-. . . Limethibitishwa na kuhakikishwa kwelikweli, tena na tena na tena, kwa ishara, maajabu, kwa mitambo, kwa—kwa—kwa Nguvu za Utendaji, kwa—kwa sayansi, kwa kanisa, kwa Mungu Mwenyewe, amethibitisha kwamba ile saa imewadia; kwa Neno, na kwa ishara na maajabu pia.

146 Ujumbe ulioidhinishwa na Mungu miongoni mwenu, kwa ishara na maajabu ya saa hii. Ujumbe kwamba Yesu Kristo si mfu, bali yu hai vile vile kama alivyowahi kuwa, na kuutuma kila mahali. Na inatimiza Malaki 4 kabisa pamoja na Maandiko mengine yote ambayo Yesu alisema yangekuwa katika siku za mwisho, yametimizwa kabisa, kisayansi, na kwa ulimwengu pia. Nayo magazeti yalichapisha picha kubwa za duara za Nuru,

ambazo zilibashiriwa hapa. Na Malaika wa Mungu, ambao wameshuka, ambao wao hawajui cho chote juu yake. Na kila mahali, kila mahali, imethibitishwa, ulimwenguni kote!

147 Linalofuatia ni kusulubishwa, nasi tunakukabili. Kama Yesu alivyosema wakati huo, "Niseme nini, 'Niokoe, Baba, na saa hii'? Lakini, la. Mapenzi Yako yatimizwe, mnaona, duniani, kama huko Mbinguni."

148 Hivyo ndivyo Kanisa linavyosema, leo, kutoka moyoni mwake, "Ati mimi nijiunge na kitu fulani...? La, Bwana, la. Mapenzi yako yatendeke, kama huko Mbinguni."

149 Angalia, baada ya Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo kuthibitishwa, wao walilikataa. Wamefanya jambo lile lile leo. Na sasa ninakaribia kufunga sasa. Na kama alivyokuja wakati huo akijitambulisha Mwenyewe dhahiri kuwa ni Neno, na ikafikia kwenye shindano la kuamua ambapo iliwabidi kuchagua Neno ama wachukue hilo shirika; imefikia kwenye jambo lile lile leo, hawana budi kuchagua Neno ama kuchagua shirika. Nao wamechukua shirika. Sasa jambo hilo linafanya nini? Katika kufunga. Yeye yuko mikononi mwa ulimwengu. Sawa.

150 Naam, fungu langu la maneno. Huo ni muda mrefu sana wa kuweka msingi, lakini sasa ndiyo kwanza nianze, mnaona. Msiamke, nilikuwa nikiwatania tu. Angalieni, hili hapa somo langu. Tunajua jambo hilo. Huko ni kuweka misingi. Tunayo hapa yamewekwa kwenye mstari mmoja hapa sasa. Hebu tulifuatilie moja kwa moja mpaka tulimalize na tuone lilivyo, tuliweke chini ya kioo.

151 Yesu yuko mikononi mwa watu. Yuko mikononi mwa kanisa. Mtamtendaje huyu Yesu aitwaye Neno lililotiwa mafuta? *Kristo* maana yake ni "Neno lililotiwa mafuta." Mnaona?

"Mtamtendaje huyu Yesu?" Pilato alisema. "Nitalitendaje? Ni-, nichukue hatua gani? Nifanyeje na huyu Yesu aitwaye Kristo?"

152 Ulimwengu ulipigia makelele kitu gani? Kanisa lilipigia makelele kitu gani? "Lisulubishe! Likomeshe! Hatulitaki tena."

153 Nitawaulizeni jambo fulani. Mnaweza kuwazia ile hatia katika mikono ya Oswald, asubuhi ya leo, yule aliyemuua Rais? Mnaweza kuwazia hukumu yake itakavyokuwa kama ikithibitishwa ya kwamba ndiye aliyetenda jambo hilo? Unaweza—ungeweza kuwazia huruma yo yote iliyosalia kwake? Damu ya Rais wa Marekani iko mikononi mwake. Unafikiria Mahakama ya Taifa...Haidhuru angejitetea kiasi gani, "Sikukusudia kufanya jambo hilo," hilo halitampa udhuru hata kidogo. Ataangamia. Kwa nini? Yeye ana damu ya Rais mikononi mwake. Ungeweza kuwazia anavyosikia? Ungetaka hilo liwe mikononi mwako? [Kusanyiko, "La."]

154 Vema, vipi kuhusu Damu ya Yesu Kristo basi? Unafikiri utasamehewa, baada ya Hilo kuthibitishwa kwelikweli? Utaliepukaje jambo Hilo? Damu Yake imo mikononi mwako, una hatia! Mwenye dhambi, utaenda wapi kutoka mahali hapa? Utafanyaje baada ya mkutano asubuhi ya leo?

155 Unafikiri, unasema, "Vema, nilitaka. . . Sikukusudia kuwa mbaya." Huenda Oswald angesema jambo lile lile.

Kama haki ya Mahakama yetu Makuu itataka haki itendeke, itaileta. Ni—ni-nini hii yetu . . . Ndiyo mkataa wa taifa letu. Taifa zima linategemea Mahakama hiyo Kuu, na hakuna kinachoweza kusalia. Yeye amevunja sheria. Hana budi kujutia jambo hilo. Haidhuru jinsi gani hakukusudia, jinsi lengo lake lilivyokuwa; ama hamna kitu juu yake; yeye atajutia jambo hilo, hata hivyo.

Kama Mahakama yetu Kuu na haki yake inadai kulipia thawabu, ni zaidi sana vipi utajikuta wewe mwenyewe kwenye Mahakama ya Mungu, utakapokuja na Damu ya Yesu Kristo mikononi mwako? "Nimtendeje huyu Yesu aitwaye Neno lililotiwa mafuta?" Umelisikia jambo Hilo. Unajua ni Kweli. Limethibitishwa kwelikweli.

156 Muuaji? Hivi ungetaka muuaji wa kimadhehebu wa Neno, kuliko Kristo asiye na hatia? Ungemsulubisha? Unge—ungethubutu kumchukua Baraba? Ungeomba upewe Baraba? Mtu ye yote angethubutuje kufanya jambo hilo, kuomba apewe Baraba, yule muuaji wa Neno; kuliko kulichukua Neno, Lenyewe, ambalo ni Uzima. Nalo limo mikononi mwako.

157 Niliposikia juu ya mauaji ya Rais Kennedy, Ujumbe huu uliingia moyoni mwangu. Nikawaza, mtu huyo atafanya nini? Na hakuna njia ya kuliepuka jambo hilo sasa. Huenda ameamka wakati huu na kutambua kinachomngojea

158 Nawe utaamka siku moja. Hapa, ama kwenye kanda, po pote ulipo, utaamka siku moja, ewe mwenye dhambi, na kutambua ya kwamba kuna Damu mkononi mwako, nayo ni Damu ya Mwana wa Mungu, nawe una hatia ya kumuua. Dhambi yako ilimuua. Kutokuamini kwako Neno Lake, kushindwa kwako kuona kujitambulisha Kwake, ukamhuzunisha Roho Mtakatifu akaondoka. Nawe unaweza kufanya nini ila kusimama kwenye Hukumu ya Mungu, ukijua kitakachokupata! Naam, damu ya John Kennedy mikononi mwa Oswald itakuwa ni jambo dogo, kuliko Damu ya Yesu Kristo mikononi mwako utakaposimama mbele za Mungu.

159 "Nimtendeje huyu Yesu aitwaye Kristo?" Pilato alisema. Yeye alikuwa amewekwa mikononi mwake.

[Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Nayo Damu ya Yesu Kristo imewekwa tena mikononi mwa kusanyiko hili. Imewekwa mikononi mwa taifa hili, na kila mahali ulimwenguni humu, ambako kanda hizi zimekuwa, na mambo ambayo yamethibitishwa na kuhakikishwa na Mungu.

Basi tumtendeje huyu Yesu aitwaye, "Yeye yule jana, leo, na hata milele"? Tumtendeje huyu Yesu? Mko tayari kuchukua mahali penu upande Wake? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

160 Pilato, na jambo lile lile alilofanya Pilato, yamesalia mambo matatu unayoweza kumtendea. Pilato alijaribu yote matatu, naye hakufanikiwa. Mbinu tatu ungeweza kujaribu kuzitumia, bali hazitafanikiwa kamwe. Pilato alijaribu kumwondoa mikononi mwake. Bali mara anapowekwa mikononi mwako, Yuko mkononi mwako. Pilato alijaribu njia tatu mbalimbali, naye akashindwa.

161 Hatuna budi kukabiliana na ukweli kwamba Yeye yumo mikononi mwetu. Tumekwishamwona katika Neno Lake. Tumemwona akijitambulisha Mwenyewe. Tunajua ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Halafu, mimi sizungumzi tu na kusanyiko hili hapa asubuhi ya leo, maana ninazungumza na watu mia sita, mia saba, labda, bali ninazungumza na mamilioni kwenye kanda hii itakayokwenda kila mahali ulimwenguni. Mnaona? Yeye yumo mikononi mwenu, katika nchi ya kanda, po pote ulipo. Unajua jambo Hilo ni Kweli. Kama hujui, basi wewe ni kipofu; huwezi kuliona Neno, wala huwezi kumwona Mungu katika Neno. Naye yumo mikononi mwako. Basi utafanya nini Naye?

162 Pilato alijaribu kumwondoa, bali inatubidi kukabiliana na mambo yalivyo. Ilimbidi Pilato kukabiliana Nalo. Yeye alijua. Alisikia.

Vema, unasema, "Sikuona hata moja ya hayo." Umelisikia, hata hivyo. Unalisikia sasa. Unaona?

Yeye alimtaka Yesu afanye muujiza, ama kiinimacho, kwa ajili yake. Bali Yeye hakuwa anafanya vitimbi; Yeye alikuwa tu anafanya yale Mungu aliyomwambia kufanya.

163 Mmesikia. "Imani chanzo chake ni kusikia." Mna imani, na mnaiondokea, kuiondoa hii mikononi mwenu. Bali hana budi kukabiliana na ukweli wa mambo, kwa vyo vyote. Yeye alifanya hivyo, na kwa hiyo sisi pia hatuna budi kukabiliana na ukweli wa mambo. Yeye ametambulishwa kikamilifu. Waza, ukiwa na Damu ya Mtu mikononi mwako!

164 Mwanadamu inampasa kuwa mwangalifu anapokuwa na damu ya mtu mwingine mikononi mwake. Angalia ndege. Rubani akitoka kwenye ndege, anapoitoa hiyo ndege, yeye huhakikisha kila chombo. Kwa nini? Yeye ana damu ya mtu fulani mikononi mwake. Kila chombo kidogo kinachoweza kuhakikishwa, yeye hukihakikisha. Anapotoka na kuigeuza ile ndege, ye—ye—yeye huizungusha mo—mo—mota, injini, na kuona kwamba imepata moto. Kisha anatupa mvuke kote kote kwake, apate kuona kwamba mlipuko uta—uta-. . .kama utaweza ku—

ku—kulazimisha, ama kuvurumisha propela, pia, kwa hewa ya kutosha kuiondoa ardhini.

Mmesimama, wengi wenu, kwenye ndege, ama kuketi chini kule, na ndege nzima inatikisika kuondoka ardhini, karibu inaruke. Yeye anaifungulia yote kabisa iliyo nayo, kuona kama kuna kasoro yo yote. Kama kuna kasoro, itatema na kushindwa ghafula. Lakini anaihakikisha tena, kama ikimbidi kuketi pale kidogo, mpaka aihakikishe tena. Na kama wakishikilia wakati wake kidogo, yeye anaihakikisha tena.

165 Jinsi Kanisa linapaswa kuwa linahakikisha tena, na tena, na tena, na tena! Tunakungojea Kuja Kwake. Tunaamka, tunakungojea kule kuondoka. Inatubidi kujichunguza kwa Neno, si kile mtu fulani alichosema. Hakikisha unajua, wewe mwenyewe, kama tukio la kibinafsi pamoja na Kristo. Jichunguze tena, na tena, na tena.

Kwa nini? Yeye ana damu ya mwanadamu mikononi mwake. Afadhali ahakikishe.

166 Vipi kuhusu daktari, kabla ya kufanya upasuaji? Tuna baadhi ya madaktari walioketi hapa asubuhi hii. Angalia, kwamba daktari, atakalofanya kabla hajaenda kufanya upasuaji. Yeye anataka x-ray. Anataka kuichunguza damu. Anataka kuuchunguza moyo. Anataka kuona kama wewe una homa yo yote, kabla hajakupa nusukaputi. Huhakikisha kila chombo; anavichemsha, kabisa kabisa, kuona kwamba havina vijidudu. Yeye hufanya kila kitu. Yeye huhakikisha tena, na tena, na tena, na tena, tena. Kwa nini? Ana damu ya mwanadamu mkononi mwake. Anataka kuwa na hakika kabisa ya kwamba kila kitu kiko sawa tu kama kiwezavyo kuwa.

167 Nawe je? Nawe je, mwenye dhambi, unaonaje juu ya jambo hilo?

Kuwa na damu ya mwanadamu mkononi mwako, jukumu kama la nahodha, yeye huhakikisha; daktari, yeye huhakikisha; na cho chote kile, mambo mengi sana ya kisayansi; unapokuwa na damu ya mwanadamu mikononi mwako, utakayofanya!

Wakati hakimu anapoenda kutoa hukumu, angalia jinsi anavyovisoma vitabu hivyo, tena na tena na tena na tena na tena, kwenye kila kipengee kidogo anachoweza kuona, kabla hajatoa hukumu. Maana, ana damu ya mwanadamu mikononi mwake, hapana budi kuwe na kitu fulani hapa kuthibitisha jambo hilo. Mnaona?

168 Na sisi je, tunapoliona Hilo limetambulishwa kinaganaga, kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele"? Yeye yuko hapa. Yumo mikononi mwetu. Yumo mikononi mwetu. Yumo mikononi mwako! Utamtendaje? "Nimtendeje huyu Yesu ambaye ni Kristo aliyetiwa mafuta?"

"Linafanya nini? Unajuaje kwamba ni Yeye?"

Ahadi ya siku hii, siku tunayoishi, kuna Maandiko mengi sana yanayosema, inchi kiasi fulani Zake zinazopaswa kutimizwa, inchi hizi za mwisho za siku hii ya mwisho. Kuna kitu fulani kinachokaa *hapa* kinachopaswa kutendeka, na hiki hapa. Ni kitu gani? Kristo yeye yule aliyetiwa mafuta, lile Neno lililotiwa mafuta! Utafanya nini Nalo? Utaliuza kwa madhehebu?

169 Basi Pilato alifanya nini? Pilato alijaribu kunawa amtoke mikononi mwake, kwa kusema... Jambo la kwanza Pilato alilofanya lilikuwa kumnawa atoke mikononi mwake, kwa kusema, "Loo, Yeye ni sawa. Hana neno." Mnaona?

170 Unasema, "Loo, maskini Pilato." Pilato, wengi wao humhesabia haki? La, la, la! Yeye alikuwa mikononi mwake. Alikuwa amesikia Ujumbe, alikuwa ameliona Neno, Naye alikuwa mikononi mwake. Vivyo hivyo Yeye yumo mikononi mwako. Hiyo ni kweli.

Alifanya nini? Alijaribu kusema, "Loo, vema, Yeye ni Mtu mzuri. Sioni hatia Kwake."

171 Kama hilo silo ji—ji—jibu la watu wengi sana leo! "Loo, Neno halina kasoro. Nafikiri liko sawa. Biblia ni sawa, bali sisi tunaamini kanisa. Madhehebu yetu hayakubaliana Nalo." Mnaona? Mnaona? Kuna tabaka moja ya watu wanaojaribu kumwosha wamwondoe mikononi mwake.

"Sioni kasoro kwenye Neno. Lilikuwa ni sawa kwa mitume katika siku zao, bali sisi tunaishi katika siku nyingine. Hatuishi katika siku za mitume, kwa hiyo basi hainilazimu kufanya kama walivyofanya mitume. Si lazima nibatizwe jinsi walivyobatizwa; ninaishi katika siku nyingine. Si lazima kutenda yale ambayo wao walikuwa nayo. Ninaishi katika siku nyingine. Roho Mtakatifu alitolewa tu kwa ajili ya kundi lile."

172 Waebrania 13:8 inamrudisha Yeye mikononi mwako tena, [Ndugu Branham anapigapiga mara tatu mimbarani—Mh.] bila kuepuka! Yeye amethibitishwa kwelikweli, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Huna njia ya kuepukia. Huwezi kumtupilia kwenye wakati mwingine. Waebrania 13:8 inahukumu mawazo yako, na kumrudisha moja kwa moja mikononi mwako tena. Kwa hiyo Yesu yumo mikononi mwako, kama tu vile alivyokuwa kwa Pilato.

Angalia. Unasema, "Lakini mimi sijui." Vema, mbona unasikiliza?

173 Pilato alikuwa mpagani. Mkewe alikuwa mpagani. Lakini Mungu, ili kulifanya lenye haki, alimtuma mwanamke huyo mle ndani na kusema, "Usiwe na neno na huyu Mtu mwenye haki." Akasema, "Nimeteswa leo." Bila shaka, ilikuwa ni asubuhi, ilikuwa usiku kucha, na masaa ishirini na manne huhesabiwa kwamba ni siku moja. "Niliteseka ndoto fulani usiku wa leo, juu ya Mtu yule mwenye haki. Usiwe na neno na jambo Hilo."

174 Sasa yeye alisema, "Vema, basi, kama hiyo ni kweli, nitamnawa tu mimwondoe mikononi mwangu." Lakini asingeweza kufanya hivyo.

Wala wewe huwezi. Mara unaposikia Kweli, huna budi kuikubali ama kuikana Hiyo. Hakuna njia . . . Naam, bwana, huna budi kufanya jambo hilo. Maonyo ya Bwana!

175 Wayahudi walipaza sauti, "Damu Yake na iwe juu yetu; kwa maana tutaamini makuhani wetu, taratibu zetu za kimadhehebu, kabla hatujamwamini."

Haya basi. Mnaona zile tabaka leo? Bali wao wote hawana budi kuikabili hoja ya Mungu. Nyote hamna budi kufanya jambo hilo, kwa vyo vyote, mpagani ama ye yote yule uwezaye kuwa. Usiyeamini, Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, vuguvugu, baridi, moto, na cho chote uwezacho kuwa, huna budi kukabiliana na hoja hiyo vivyo hivyo. Kama unataka kufanya jambo hilo, ama hutaki, Liko mikononi mwako. Hiyo ni kweli kabisa.

176 Kisha kuna wale wanaojaribu mbinu ile nyingine ya Pilato kuepa hoja, kumpeleka kwa Kaisari mwingine. Mnaona?

Pilato alisema, "Sasa ngojeni kidogo. Si—si—si—sitaki uhusiano wo wote na jambo Hilo. Mi—mi—mi—mimi . . . Naam, Yeye ni mtu mwenye haki. Si—sitaki uhusiano wo wote Naye. Loo, ni—ninaamini yale niliyosikia. Sijamwona kamwe akifanya muujiza, bali kuna mashahidi wengi sana kwa ajili Yake. Ni—ni—ninaamini Yeye ni Mtu mwenye haki. Ni Mtu mzuri, mnaona, lakini mimi—lakini mimi—sitaki uhusiano wo wote na jambo Hilo, mimi mwenyewe. Mi—mi—mimi tu . . . Nitamnawa tu nimwondoe Yeye mikononi mwangu. Nileteeni maji. Nyote mnanishuhudia hapa." Naam. Bali Mungu alikuwa anashuhudia, pia. Alikuwa mikononi mwake.

177 Na vivyo hivyo Yeye yuko mikononi mwenu. Mnaona, ninyi, mnajua ninalozungumzia. Mnaona? Si ninyi tu, lakini kanda hii. Yeye yumo mikononi mwenu. Mtamtendaje, huyu Yesu aitwaye Kristo? Kristo ni Neno Lililotiwa Mafuta. Mnaona? Mtalitendaje? Ni Ujumbe wa Saa hii. Siku hiyo iko hapa, imethibitishwa kwelikweli na Biblia pamoja na Mungu. Utalitendaje? Utaiepaje hoja hii sasa? Utaiepukaje? Yeye yumo mikononi mwako! Na kesi ya Oswald itakuwa ndogo, ukilinganisha na yako, ingawa wewe ni mhudumu ama cho chote kile.

178 Hao Wayahudi walikuwa makuhani, na marabi, walimu, watu watakatifu; bali alikuwa mikononi hata hivyo. Yeye alikuwa Neno, hoja ya Mungu kwa ajili ya siku hiyo, nao wakakosa kuliona Hilo. Ni wateule tu walioliona, wale walioliamini Hilo.

179 Sasa wote hawana budi kukabiliana na hoja hiyo. Katika kila wakati imekuwa hivyo, kila wakati. Wakati wa Hawa na

Adamu, na kuendelea hadi wakati wa Nuhu, na kuendelea hata kufikia wakati wa Danieli na Belshaza na Nebkadreza, na kuendelea hata katika wakati wa Kristo, na kuendelea hadi katika saa ii hii tunayoishi, imekuwa ni vile vile, swala la Neno limetokea. Si kanuni yao ya imani, wala si madhehebu, si mafundisho ya sharti, lakini, swala la Neno limekuwa kinyume na mambo hayo. Kwa hiyo, sasa, Hilo limo mikononi sasa.

180 Kisha wale wanaojaribu mbinu nyingine ya Pilato, kumwondoa, kwa kumpeleka kwa mtu mwingine. Pilato alisema, "Naam, mnajua nini? Nitamwondosha tu mikononi mwangu. Nitamnawa tu nimwondoe mikononi mwangu kwa maji haya. Kwa hiyo mimi nitanini hii tu . . . Sina budi kumtenda jambo fulani. Kwa hiyo nitafanya nini? Nitampeleka huko kwenye makao makuu, pamoja na askofu." A-ha. Naam.

Hivyo ndivyo wanavyojaribu kufanya leo. Mnaona? Walimpeleka kwa Kaisari fulani. Hilo halikumwondoa kwenye mikono ya Pilato, haimwondoi Yeye kwenye mikono ya mtu ye yote. Ilifanya nini? Lilimrudia mwenyewe. Hurudi moja kwa moja kwa mtu binafsi.

181 Unasema, "Vema, ningetaka, ningefanya hivyo. Ningelikubali kama madhehebu yangu yangelikubali Hilo."

Madhehebu yako yamo katika Baraza la Makanisa, yamehukumiwa! Watalipokea namna gani? Linakurudia, moja kwa moja kwako. Si yale yasemayo madhehebu yako; ni, je! wewe unasema nini? Yamelikataa; basi utalitendaje? Hilo ndilo jambo linalofuata. Unaona? Jambo hilo halimwondoi Yeye mikononi mwako.

Yeye amethibitishwa kikamilifu. Ametambulishwa kikamilifu, Neno la wakati huu, ahadi ya wakati huu. Si ahadi ya wakati wa Luther; hilo lilikuwa Ndilo wakati huo, hilo lilikuwa Neno katika wakati wa watengenezaji. Kama vile, ninyi nyote mliosikia zile Muhuri Saba, wakati wa wale watengenezaji ulipokwisha, yule Mwenye Uhai mwenye uso kama wa mwanadamu (madhehebu) alitokea; bali huu ni uso wa tai, yule Mwenye Uhai aliyetoka akaenda kutoa sai leo.

182 Basi ni nani angethubutu kusema hilo halikuwa Neno la Mungu lililotiwa mafuta, wakati Yeye alipolitabiri hapa, kisha akanituma kule Arizona na kulirudisha moja kwa moja, hata na sayansi na cho chote kile, na kulithibitisha kwamba ni kweli! Kitabu *hiki* tayari kimefunguliwa, hiyo ni kweli, tunangojea tu ile Muhuri ya Saba kutambulishwa ya kule Kuja kwa Kristo.

183 Vema, Yeye yuko mikononi mwako. Huna budi kumtendea jambo fulani. Usimwondoe. Naam, bwana. Katika kundi hili, ningetaka kusema, "kumpokezana Yeye kwa mtu mwingine."

Kama madhehebu yangu yangelikubali Hilo, Ndugu Branham, ninge-—ningelikubali. Lakini, unaona, mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili." Yeye aliishi katika wakati wake;

huyo si wewe. Ni zamu yako sasa. Angalia mahali palipomlazimu kutoka, kusudi aje akatende yale aliyokuwa. Na wewe je? Vema.

184 Angalia. Unasema, "Mama yangu alikuwa Mpentekoste. Alifanya *kadha na kadha*. Yeye alitoka katika madhehebu." Lakini ninajaribu kuzungumza nawe sasa. Na wewe je? Mnaona?

Katika kundi hili, tunawaona wengi wenye elimu. Naam, ninajua nitawaudhi watu hapa, bali sifanyi hilo makusudi. Kama ninafanya jambo hilo, basi ina—inanibidi kushuka madhabahuni, nikitubu. Ninasema jambo hili katika upendo wa kiungu.

185 Yesu, wakati Yeye aliposimama pale, na hao Mafarisayo; ilimbidi kusema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi; kazi zake mtazifanya." Hata hivyo akawaombea amani na rehema, pale msalabani, wale waliomsulubisha. Mnaona, Yeye hakuwakasirikia. Alisema, "Enyi kizazi cha majoka." Mnaona? Mnaona? Kila kitu, aliwalaani kwa kila kitu alichoweza, mnaona, kisha akawaombea pale msalabani. Mnaona? Si kwamba alitaka kufanya jambo hilo; haikuwa hivyo, bali iliwabidi kuona kosa walilokuwa wanafanya.

186 Nami ninasema jambo lile lile leo, katika kundi hili la "kusukumizia mtu mwingine lawama," ama kitu fulani tunachokiita kule jeshini, "kumpitishia dolla mtu mwingine." Tunajaribu kulisukumiza, kama Adamu na Hawa walivyofanya.

Hawa alijaribu. Adamu alisema, "Mwanamke uliyenipa," na hilo halikuwa la udhuru kwake. Mnaona? Yule mwanamke alisema, "Nyoka alinidanganya. Yeye . . . Yeye ndiye aliyenijua kimwili. Alinidanganya. Alifanya jambo *hili*." Hilo halikuliondoa, hata kidogo. Wao walielekea moja kwa moja hukumuni, hata hivyo. Naam, bwana. Vema.

187 Hawawezi kuipokezana, mmoja . . . Hawezi kusema, "Kama madhehebu yangu yangeamini Hili, ni—ninaamini pia. Lakini, nimekuwa katika madhehebu haya." Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Wayahudi walikuwa na jambo lile lile, nawe pia.

188 Basi, angalia, wengi katika jambo hili, tunaona watu wazuri waungwana katika kundi hili. Sasa sikilizeni kwa makini.

Mnaona, ustaarabu, tunachoita ustaarabu leo, ndio Shetani aliompa Hawa, hekima kidogo. Kasema, "Macho yako hayajafunguliwa, hata huelewi na jambo Hilo lote." Yeye alijua Neno, na hilo lilitosha. Alimwona Mungu akithibitisha Neno hilo, na hilo lilipaswa kuwa sawa. Yeye alikuwa akimweka katika Uzima wa Milele, mradi tu alikaa na Neno hilo. Alipolivunja Neno hilo, yeye alikuwa na ahadi ya Mungu kwamba angekufa siku hiyo ambapo alilivunja. Basi, alipolivunja, akafa. Hiyo ni kweli.

189 Tuna Neno la Mungu lililothibitishwa hapa, likithibitisha, kuhakikishwa na Roho, ya kwamba Yeye ametupokea na kutupa Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tumebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Injili ile ile, ishara zile zile, maajabu yale yale, huduma ile ile, hata Nguzo ya Moto ile ile ikionekana mbele zetu, ikionyesha ishara na maajabu. Hakuna udhuru, mahali po pote.

Na hilo ndilo hasa Biblia ilisema lingetukia katika siku za mwisho, na mwito kutoka Malaki 4, "kuirudisha Imani ya watoto iwaelekee baba zao tena." Na mara baada ya jambo hilo, walio waovu walitembea...ama wenye haki walitoka wakatembea juu ya majivu ya walio waovu; ulimwengu mzima ulikuwa uteketezwe. Nazo atomi zinaning'inia juu kule ng'ambo, hayo mabomu kwenye vile vibanda.

190 Mnaona kile Ujerumani ilifanya mara walipoona kwamba Rai-...Rais ameuawa? Walikusanya jeshi lao pamoja upesi sana, kwa maana hilo tu ndilo lililokuwa likiizuia Urusi wasipige mabomu hapo. Nao wakapiga... Kennedy ndiyo kwanza awapelekee habari, ya kwamba, mara watakapofanya jambo hilo, kwamba angewafutilia mbali awatoe duniani, moja kwa moja kutoka Ujerumani. Mnaona? Nao walifikiri wangeweza kuiteka, bali wakati wake haukuwa umewadia bado, mnaona. Mnaona?

191 Tunawaona wahubiri na wainjilisti walio werevu, wenye elimu, wakijaribu kusukumia Hilo kwa mtu mwingine. Mnaona?

Kwa nini, kwa nini Pilato hakusema, "Vema, ngoja kidogo, Mtu huyu...mke huyu amekuja akaniambia, nami nimesikia shuhuda nyingi Zako. Unajua, mimi—mimi ninataka. Ningetaka kujua. Nifanye nini nipate Uzima wa Milele, Bwana? Wewe umo mikononi mwangu. Nifanye nini?" Vema, yeye angesema—angesema...Alisema, "Hivi—hivi Wewe ndiye Masihi? Hivi—hivi Wewe ndiwe—ndiwe Mfalme wa Wayahudi?

192 Akasema, "Hivyo ndivyo ulivyosema. Ulisema jambo hilo."

"Ama, tuambie, kwa hakika, Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?"

Yeye akasema, "Kwa kusudi hilo nilizaliwa."

Yeye akasema, "Siwezi kuona hatia ndani Yake." A-ha. "Vema, nitamnawa tu nimwondoe Yeye mikononi mwangu."

193 Yeye akamjibu, lakini hakuweza kupokea jambo Hilo. Kwa nini? Lingeishusha sifa yake. Kwa hiyo akafikiri angemtuma kwa mzee wa jimbo, aone kile alichofanya juu ya jambo Hilo. Mnaona?

194 Ni jambo lile lile leo, swala hilo linatokea tena. Utalitendaje, lile Neno? Inakubidi kufanya nini, kumuuliza mzee wa jimbo, ama askofu, ama mtu fulani, kama unaweza kubadilisha azimio lako la ubatizo, kama unaweza kufanya jambo *hili*, ama kufanya

*hili*? Unaona *hivyo*, na, "Bila shaka, sivyo ulivyo." Unarudi moja kwa moja kwako. Kama ukifanya hivyo, utafukuzwa. Mnaona?

195 Lingeshusha sifa ya hao watu. Naam, wao—wao wanafikiri . . . Nayo halmashauri ya madhehebu isingestahimili . . . Kama—kama Pilato akimsukumia Kaisari jambo Hilo; Wasingelistahimili jambo Hilo. Kaisari alilirudisha kwenye mkono wa Pilato. Kwa hiyo wao wanajaribu kumpokeza kwa wakuu wao—wao wa madhehebu yao, nalo halifanikiwi. Mbinu hii haijafanikiwa kamwe, wala haitafanikiwa. Haikufanikiwa kwa Pilato; haitafanikiwa kwako; haitafanikiwa kwa mtu mwingine. Naam, pili, jambo unaloweza kufanya ni . . .

196 La tatu, hasa, ni kumkubali ama kumkataa Yeye. Huwezi kumnawa umwondoshe mikononi mwako. Huwezi kumsukumiza kwenye shirika lingine, wala kitu kingine cho chote. Huna budi kukabiliana na kisa hicho. Basi unaweza kufanya nini?

Kama vile Pilato, alivyosimama na jambo lilo hilo, akasema, "Nipeni maji, nitalinawa litoke mikononi mwangu, kuthibitisha!" Aliporudi, bado alipaswa kutoa hukumu; halikumpa udhuru. Alijaribu kusema, "Vema, mimi, kama siwezi kumwondoa mikononi mwangu, nitamweka kwenye mikono ya Kaisari." Nalo likarudi, moja kwa moja kwake.

197 Linakurudia wewe, pia, kama mtu binafsi. Utafanya nini? Si kile alichofanya mama, kile alichofanya baba, kile anachofanya mchungaji, kile anachofanya Ndugu Branham, cho chote kile; Liko mikononi *mwako*! Utafanya nini juu Yake, ukiwa na huyu Yesu aitwaye Kristo? Maana, una Damu mikononi mwako, Nayo ni Damu ya Mungu. Basi utafanya nini? Utakuwa na hatia ya kule kusulubisha. Unaona?

198 Unaweza kumsulubisha, kukubali kanuni yako ya imani ama cho chote unachotaka kufanya, ama kusema, "Vema, nitaliondoa kwangu tu. Sitakuwa na uhusiano wo wote na upuzi huu wa kanisa." Huwezi kufanya jambo hilo. Yuko mikononi mwako. Hiyo ni kweli. Huwezi kufanya jambo hilo. "Nitasahau tu jambo hilo lote." Huwezi kafanya jambo hilo. Lingali mikononi mwako. "Vema, nitasema tu, 'Mchungaji wangu alinifundisha jambo *hili*.'" Linakurudia, moja kwa moja. Ni kwa ajili yako. Wajua. Naam, unaweza ukampokea ama unaweza kumkataa, njia yo yote tu unayotaka kutenda hilo. Ati nini? Lazima lije kwa mojawapo.

199 Vipi sasa? Kama Yesu alivyowaambia Mafarisayo hawa, Yeye alisema, "Kwa kuwa ninyi ni Mafarisayo vipofu," mnaona, Ambaye angesema jambo lile lile leo, "enyi walimu vipofu wa dini, mnaweza kuutambua wakati wa ukomunisti. Mnakipiga vita kitu hicho sana, nanyi mwajua ya kwamba Mungu alikiinua kitu hicho hicho kiwaamgamize ninyi." Mnaona, bila kuyajua Maandiko. Mnaona? "Ninyi, mnaweza kutambua ya kwamba

ukomunisti utauteka ulimwengu. Mnaweza kuona jambo hilo. Mnaweza kutambua jambo hilo."

200 Mahubiri yetu yote ni juu ya ukomunisti. "Ufukuzeni Ukomunisti!" Ninasikia jambo hilo mpaka ninachoswa kabisa na kulisikiliza. Mimi ninaupinga, pia. Bila shaka, ninaupinga. Bali mimi ninampinga zaidi mwanamume ama mwanamke anayemkataa Yesu Kristo, aliye Neno. Ama, kama wewe ni mhubiri ama cho chote ulicho, wewe unawiwa na Kristo kuliko mkomunisti huyo anavyowiwa. Yeye hana habari na hajui lo lote kuhusu jambo Hilo. Wewe unapaswa kujua. Mnaona? Mnaweza kuutambua wakati wa ukomunisti, bali hamwezi kuitambua ishara ya siku mnayoishi.

201 Yesu aliwaambia Mafarisayo, kasema, "Enyi wanafiki!" Kasema, "Mnatoka nje na kuangalia anga, na mnasema jua ni jekundu tena kumetanda, kesho kutakuwa na dhoruba. Kama kuna kianga," kasema, "mnasema kesho kutakuwa na kianga." Kasema, "Mnaweza kuzitambua ishara za zamani hizi, ama ishara za mbingu na hali ya hewa, bali ishara za zamani hizi hamzijui." Huyo hapo, Masihi, nao wakimkataa.

Nasi daima tunazungumza juu ya wakomunisti na baadhi ya mambo haya, lakini, ishara ya zamani hizi, hatuipati. Mnaona? Tunapuuza jambo hilo, tunaliacha hilo. Wanaungana sasa hivi katika kutokuamini, nao wanalipokea jambo hilo, bali wanashindwa kufahamu na kuona ishara ya zamani hizi ambazo Biblia ilisema zingekuweko.

Mmelifahamu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sina budi kufunga, upesi sana sasa. Tumechelewa, mnaona.

202 Kama walivyofanya baba zao, ndivyo wanavyofanya, jambo lile lile leo. Naam, uamuzi umekwisha kufikiwa. Hauna budi kufikiwa. Huna budi kuufikia, kwa njia fulani. Mnaona? Kusulubiwa kwa Neno tena, ama utafanya nini? Kusulubiwa kwa Neno kumewadia. Kusulubisha na kukomesha Neno lililothibitishwa, kwa—kwa ajili ya madhehebu, kama alivyofanya Pilato, kujaribu kumpokeza mtu mwingine. Basi wewe, kama mtu binafsi, utafanya nini na Neno lililotiwa mafuta ambalo linaitwa Kristo?

Yeye yule jana, Kristo yeye yule aliyelitia mafuta Neno katika siku za Nuhu. Kristo yeye yule, ule—ule Mti uliokuwa katika Bustani ya Edeni; ambao Hawa aliacha, kula kutoka kwenye Mti huu wa Uzima, akachukua mti wa hekima; mwanamume, mwanamke aliuacha Mti wa Uzima, apate kula ule mti wa mauti. Zamani za Nuhu zilifanya jambo lile lile. Katika siku za manabii, walifanya jambo lile lile. Katika siku za Kristo, walifanya jambo lile lile.

Nao hawa hapa leo. Kwa kila mmoja akinena habari za wakati wake, na, wakati jambo hilo lilipotimizwa, kila wakati walipochukua hoja zao za kimadhehebu, na kadhalika, na

hekima ya ulimwengu badala ya Neno lililotiwa mafuta la Kristo. Utafanya nini, kama mtu binafsi?

203 Pilato hakumwondoa Yeye mikononi mwake. Nina—ninamaliza, kwa hiyo iweni watulivu sana kwa dakika moja tu. Pilato hakumwondoa kamwe mikononi mwake. Wala wewe hutamwondoa, jinsi alivyofanya, kujaribu moja ya njama hizi. Hakufanya jambo hilo kamwe. Mnajua kilichompata Pilato? Alirukwa na akili. Ilifikia mahali ambapo yote aliyoweza kusikia ilikuwa ni kule kusulubishwa. Yote aliyoweza kusikia ilikuwa ni ile hasira, hata hatimaye akawa wazimu.

204 Nao wana hadithi ya kubuniwa huko mbali Norway, ama si-. . .samahani. Huko Uswisi; ambako, nilikuwa kule, mmishenari. Wao wanadai maelfu hukusanyika kule, kutoka ulimwenguni kote, kwenye Ijumaa Kuu; shimo la maji ambapo Pilato alijiiua. Hatimaye alijitupa kwa nguvu akafa kwenye kidimbwi hiki cha maji. Nao wanadai ya kwamba kila Ijumaa Kuu, kwenye saa tisa alasiri, hayo maji hugeuka yakawa samawati, nayo yanachemka kutoka mahali ambapo mwili wa Pilato ulilala. Yeye alilikataa Hilo. Kungali kuna Damu mikononi mwake. Naye alikataa, akakataa; yale maji.

Huwezi kumnawa ukamwondoa Yeye mikononi mwako. Hakuna maji, hakuna sabuni ya asili, ambayo inaweza kuisafisha Hiyo. Yeye yuko mikononi mwako. Utamtendaje?

205 Hili hapa jambo pekee unaloweza kufanya. Kama huwezi kunawa ukamwondoa mikononi mwako; huwezi kumpokezana kwa kitu kingine; huwezi tu kuliepa kama hadithi za kubuniwa. Hakuna njia ulimwenguni. Jambo pekee unaloweza kufanya ni kulikubali, moyoni mwako. Hiyo ndiyo njia ya kumwondosha. Mwondoe mikononi mwako ukamweke moyoni mwako, ama umwache mikononi mwako kisha ukasimame Hukumuni. Hilo ndilo jambo pekee unaloweza kufanya.

Mwisho wa Pilato ulikuwa wa kutisha.

206 Neno linasema ya kwamba hawa wanaomweka mikononi mwao. . .Nilikuwa nilisome. Bali ilisema, "Waliililia miamba na milima. Waliomba, bali maombi yao yalikuwa yamechelewa mno." Mnaona? Walilia, "Tufiche na uso wa Yeye aketiye kwenye Kiti cha Enzi, na kutoka kwenye hasira ya Mwana-Kondoo ambaye ata-. . .na Kondoo, Uzima wa Mwana-Kondoo ajaye. Kwa maana, ile Siku kuu ya Hukumu imetimia, na ni nani atakayeweza kuistahimili?"

207 Mnafikiri Oswald atafanya nini sasa wakati anapoenda mbele ya Mahakama Kuu, na kuona hayo macho yenye hasira ya jo—jopo la waamuzi na wote wameketi pale? Yeye anajua litakalotukia. Itakuwa aidha ni chumba cha gesi, ama kitanzi kinachoning'inia pale, ama kitu fulani. Hana budi kukabiliana na jambo hilo.

208 Lakini vipi kama ukienda kule nje huku hiyo Damu imo mikononi mwako, kwa kukataa? Nawe unajua ya kwamba kuzimu kuko mbele yako, maangamizi ya Milele; kuililia miamba na milima; bali waliomba, kwa kuwa maombi yao yalikuwa yamechelewa sana.

Katika Waebrania 10, "Kama tukifanya dhambi kusudi." *Dhambi* ni "kutokuamini." "Kama tukikosa kuamini kusudi baada ya kuipokea ile Kweli, ule ujuzi wa ile Kweli." Si lazima uupokee; ujue tu habari Zake. Si lazima uwe Nayo, wewe nini hii tu. . . Lo, la. Mnaona? Haikusema, "baada ya kuipokea ile Kweli."

> . . . *tukifanya dhambi kusudi baada ya* sisi *kuupokea ujuzi* kwamba ni *wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi,*
>
> *Bali . . . kuitazamia hukumu kwenye kutisha*, *ukali wa moto . . . tayari kuwala wao wapingao*.
>
> . . . Kwa maana Mungu alisema, *Kupatiliza kizazi ni Kwangu*, *mimi nitalipa*, asema—asema Bwana.

209 Kama tukikosa kuamini jambo Hilo, kusudi, baada ya kupewa ile Kweli, hakutakuweko na rehema tena. Hakuna rehema nyingine itakayotolewa.

Ewe mchungaji, unayesikiliza kanda hii, vipi kuhusu jambo hilo? Ewe mshiriki wa kanisa, unayesikiliza kanda hii, vipi kuhusu jambo hilo? Utafanya nini, kama tukikosa kuamini Hilo kusudi? Huwezi kulinawa uliondoe mikononi mwako. Huwezi kulisukumia makao makuu. Litarudi, moja kwa moja kwako. Umelisikia. Na wewe je? Utasimama vipi kwenye ile Siku?

Yeye yuko aidha mikononi mwako ama moyoni mwako, moja au jingine. Mungu na atusaidie.

210 Kama—kama unaweza tu kuwazia kule kuua, na kile ambacho hakina budi kuwa kinaendelea katika moyo wa mtu yule. Amefanya nini? Yeye aliamka amechelewa sana, baada ya yeye tayari kufanya jambo hilo.

Angalia, yeye alikuwa na nafasi. Alizaliwa Mmarekani huru. Yeye alikuwa Mmarekani. Bali alitaka kuuza haki zake za mzaliwa wa kwanza, apate kuwa Mrusi, nalo likamrudia. Yeye alioa msichana wa Kirusi. Sasa yeye ni mfuasi mwenye uhuru wa mawazo wa chama cha kikomunisti cha Cuba.

Uhuru wa mawazo, "Mimi huwaza nitakavyo." Huna wazo linalokuja. Utamtendaje Yesu aitwaye Kristo? Wewe si mwenye uhuru wa mawazo. Hakuna uhuru wa mawazo. Nia iliyokuwa katika Kristo na iwe ndani yako.

Na tuombe.

211 Wazeni mawazo haya, "Kukiwepo sifa yo yote, kukiwepo wema wo wote, litafakarini hili." Katikati yetu asubuhi hii, na

kwenye kanda hii, pia, ninazungumza. Kama uko hapa asubuhi ya leo, nawe unajua ya kwamba huko sawa na Mungu, wala hujazaliwa kwa Roho Wake, na Mungu ame-. . .

Unasema, "Vema, nimekiri." Hilo silo ninalozungumzia. Je! Mungu amekubali jambo hilo? Unaweza kusema, "Naam, mimi, nimekiri, na kadhalika. Naam, ninaamini." Vivyo hivyo Pilato, "Nimekiri, hakika, 'Nimtendeje huyu Mtu mwenye haki?'" Huwezi kumnawa umwondoshe mikononi mwako namna hiyo. La, la.

212 Utamtendaje? Iwapo wewe si Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, huku Roho Mtakatifu akiishi ndani yako, akiyachochea Maisha yako, basi mbona usilipokee Hilo sasa? Hutalinawa uliondoe Hili mikononi mwako. Hutasikia kamwe mwisho wa Ujumbe huu. Litapiga kengele wakati wote mpaka uuingize Ujumbe moyoni mwako, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

213 Katika kusanyiko hili linaloonekana asubuhi ya leo, kuna watu walio hapa watakaotambua ya kwamba, ya kwamba wamekosea, nanyi mngeinua mikono yenu. Hatuna nafasi kwa ajili ya wito wa madhabahuni, mahali hapa pamejaa sana. Lakini sema tu, "Niombee, Ndugu Branham. Mungu anisaidie." Mungu akubariki, ninauona mkono wako. "Ni, ninataka, sasa. Papa hapa nataka, mbele za Mungu, Yeye anajua ya kwamba nina hatia, nami ninatambua nina hatia. Ni—ninataka aondoke mikononi mwangu; ninamtaka moyoni mwangu. Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Bwana akubariki. Ninaona, katika kiasi hiki cha watu hapa, labda mikono arobaini, hamsini hapa iko juu.

Akwita leo,
Akwita leo,

Wazia jambo hilo sasa, huyo ni Yeye akiita. Yesu anaita. Huyo ni Yeye akinena nawe.

214 Hivi umefanya dhambi sana, hata moyo wako umekuwa mgumu sana, hata hutaweza, huwezi kulisikia tena? Wakati mmoja, kama mvulana mdogo ama msichana mdogo, ulilisikia. Ulikuwa na shauku ya kufanya jambo hilo, bali ukaliweka kando, nawe ukawa mgumu tu na mgumu kwenye mikato hiyo na mivuto. Hivi limeenda mbali sana hata huwezi kulisikia Hilo tena? Hivi unasimama ambapo . . . nini hii yako . . . kwenye mahali kama pale Oswald aliposimama asubuhi ya leo, unapopajua? A-ha! Unawezaje kufanya jambo hilo?

Kutakuwa na mwingine kabla hatujafunga nami nitaomba dua? Po pote tu pale kwenye jengo, ambaye hukuinua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, tangu tu uliposema maneno ya mwisho, na—najisikia hivyo." Mtu ye yote, huko nje, ukumbini, kwenye madirisha, po pote pale, haidhuru. Nini hii tu . . .

215 Mungu akubariki, bibi mdogo. Mungu akubariki, bwana, wewe. Nilikupata. Yeye yuko . . . Mungu akubariki, bibi. Mtu mwingine? Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, hapa. Na Mungu akubariki kule, mvulana mdogo, msichana mdogo. Naam, Bwana akubariki. Kule nyuma, bwana. Naam.

Sasa hebu tuliwazie jambo hilo sasa. Nawatakeni mfanye jambo hili huku tukiuimba huu polepole, *Yesu Akwita*. Sasa nawatakeni kusema tu, "Bwana, nirehemu mimi, mwenye dhambi, ama ajifanyaye. Mimi ni mfuasi wa kanisa, Bwana, bali na—na—nakutaka Wewe. Ninakutaka Wewe. Nisaidie! Nita—nitakutumikia Wewe. Ninaahidi jambo hilo, sasa hivi. Nimeuinua mkono wangu, kwamba nakutaka. Sasa Wewe uinue moyo wangu, ili kwamba nikupokee, nami nitakupokea moyoni mwangu." Tunapoimba ubeti huu tena, utafanya jambo hilo?

Akwita leo,
Akwita leo,

216 Sasa ombeni mnavyotaka. Ombeni sasa. "Yesu akwi- . . . " Huyo ni Yeye anenaye. Hiyo ndiyo sababu uliinua mkono wako.

. . . kwa upendo akwita leo.

Yesu akwita, Ee isikilize Sauti Yake;
Msikilize . . .

Hivi sasa, msikilizeni Yeye. Semeni, "Bwana, mimi nina hatia. Damu yako imo mikononi mwangu. Mimi ni mwenye dhambi. Siitaki hapo tena. Siwezi kuinawa ikaondoka; nimejaribu jambo hilo, kwa miaka kadha. Mimi sitakukataa kama alivyofanya Pilato, na kujaribu kukupeleka kwa mtu mwingine. Ninakutaka. Njoo moyoni mwangu, sasa hivi, Bwana. Nakupokea. Ninakuona ukisimama moja kwa moja mbele yangu, kama sanamu inayosimama pale; kwa imani ninakuja moja kwa moja Kwako, nikijua ya kwamba utanisamehe. Nami . . . Utakuwa moyoni mwangu, tangu sasa na kuendelea."

. . . leo, (kila mtu aombe)
Yesu akwita,
Anakwita kwa upendo leo.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Yesu Akwita*—Mh.]

217 Baba wa Mbinguni, huo Ujumbe mdogo umekwisha. Na sasa, maamuzi, mahakama yameketi asubuhi ya leo. Malaika wamekusanyika chumbani. Roho Mtakatifu mkuu hapa akitoa ushuhuda kwamba Yesu Kristo yuangali hai. Yeye alikuwa chemchemi ya Uzima wa Milele. Kaburi halikuweza kumzuia, wala kuzimu kusingeweza kumzuia. Yeye alipaa juu; akiwa huru kutoka kuzimu, akiwa huru kutoka kaburini. Naye anasimama kati yetu, leo.

Nazo kanuni zetu na madhehebu vimewafunga watu wetu wengi, Bwana. Dhambi imewafunga, bali leo wao wanataka kuwa huru. Wao wanasimama kama Pilato, na,

badala ya kujaribu kumsukumia mtu mwingine, wao wameiinua mikono yao, "Ingia moyoni mwangu, Bwana Yesu. Mimi sitakunawa nikuondoe kwangu tena. Siwezi kufanya jambo hilo. Ungali katika mikono yangu. Ndiyo kwanza niisafishe na kuisafisha, Nawe usingeweza kutoka, bali sasa ninakupokea. Ninakutaka Wewe maishani mwangu, nami nakupokea maishani mwangu. Bwana, nipokee katika Ufalme Wako, kwa kunisamehe dhambi zangu, kisha unipe imani kuamini ya kwamba Wewe unanipokea, Baba." Tujalie. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba.

218 Na sasa huku mkiinamisha vichwa vyetu. Imani, kwa imani . . . "Basi, Mungu, nisaidie kuwa mwaminifu. Lakini nikijua ya kwamba Wewe uliahidi kwamba . . . "

"Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe. Nami nitampa Uzima wa Milele, Nami nitamfufua katika siku za mwisho. Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Yeye alisikiaye," tafsiri halisi na ya kweli ya Yohana Mtakatifu 5:24 pale, ni, "yeye afahamuye, ambaye analipokea Neno Langu. Yeye alipokeaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataitwa Hukumuni." Hutakuja Hukumuni kama Oswald atakavyokuja. "Bali umepita," na msamaha wa bure, "kutoka mautini kuingia Uzimani."

219 "Bwana, sijui jinsi gani, sijui kwa nini, lakini—lakini naamini limetukia. Ninaamini jambo hilo, moyoni mwangu, kutokuamini kwangu kumeondoka. Ninaweza kusema kwa uhuru "amina" kwa kila Neno unalosema, nami nalikubali sasa hivi. Ninaliamini."

220 Sasa huku vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa. Ninyi mnaoamini jambo hilo, mlioinua mikono yenu dakika chache zilizopita; na kwa imani mnaona sanamu ya Kristo imesimama pale, ambayo mwapaswa kuwa ndani yake. Mnatembea sasa kwa imani, aminini ya kwamba dhambi zenu zimesamehewa. Na tangu leo na kuendelea, mko tayari kwa ubatizo wa Kikristo, nanyi mko tayari sasa kuenenda katika Kristo. Basi mngeweza, kama ushuhuda Kwake, kuinua mikono yenu tena, mkaseme, "Kwa imani ninaamini jambo Hilo kwa moyo wangu wote"? Mungu akubariki. Hilo ni sawa. "Sasa ninalikubali Hilo. Ni—ninalikubali; hamna kitu ninachoweza kufanya." Mungu akubariki. Ilionekana kama kila mtu niliyemwona. "Sasa nakubali."

221 Mnaona, wewe si mzuri, hujakuwa mzuri kamwe, huwezi kuwa mzuri, bali Yesu aliwafia watu wasiofaa. "Inanibidi kufanya nini, Ndugu Branham?" Kubali tu alilofanya, kubali tu alilokufanyia. Na sasa kwa kuliamini jambo Hilo na kulikubali . . .

Sasa naamini, mchungaji, kidimbwi kitakuwa wazi. [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Ubatizo utakuwa tayari, kama mkitaka kubatizwa.

Kama umechukua vyeo, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," wewe kweli . . . Ninasema jambo hili kwa kicho na heshima, lakini, nionavyo mimi, hujabatizwa bado. Hujabatizwa, kwa maana hujafanya alilosema.

222 Yeye alisema, "Muwabatize katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Kama vyeo hivyo vilitajwa tu juu yako; Yeye hakusema kamwe, "Nendeni mkavitaje *vyeo* hivi; nendeni mkayaite *majina* haya." Jambo hilo halikutendwa kamwe katika Biblia. Halikufanywa namna hiyo kamwe. Ilikuwa, batizeni jinsi Yesu alivyosema, "Katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ambalo ni Yesu Kristo.

223 Petro, akiwa na zile funguo, alisema jambo lile lile; kila mtume mwingine, Kanisa zima; hata lile Baraza la mwanzoni la Nikea wakati Kanisa Katoliki la Kirumi lilipounda madhehebu, likakubali vyeo badala ya Jina. Aidha wewe umebatizwa katika mafundisho ya sharti ya madhehebu ya Kirumi, ama umebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, moja au jingine. Liko mikononi mwako; huwezi kuliondoa kwa kunawa. Liko hapo.

Mmelikubali sasa. Nitawaulizeni, wakati—wakati mpiga kinanda na mpiga piano wanapoufungua ule wimbo unaojulikana sana.

Yesu kwa imani,
Nakutumaini,
Peke Yako,
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni wako kabisa
Tangu leo!

224 Mtu ye yote asiondoke jengoni. Simameni kwa uchaji tu sasa, hebu na tumwinulie mikono Yetu sasa.

Yesu kwa imani (Naye ni Neno)
Nakutumaini,
Peke Yako,
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni wako kabisa
Tangu leo.
Niwe kabisa, kabisa na kabisa, Wako!
Sasa nayasalimisha maisha yangu.

225 Maji yatakuwa tayari mnamo dakika chache. Kama huwezi kufanyiwa ubatizo sasa, tutabatiza tena usiku wa leo.

Wazia jambo hilo, alasiri yote, "Mikononi mwako." Liondoe. Njia pekee unayoweza kutenda, ni, kuoshwa katika Damu ya

Yesu, Kristo, Ambaye ni . . . Mnaona? Naam, bwana. Kumbukeni jambo hilo sasa tunapoinamisha vichwa vyetu. Mwangalieni Yeye sasa.

Hapa nazunguka . . .

226 Uamuzi uko moyoni mwako sasa. Yeye yuko hukumuni. Neno liko tayari kusulubishwa. Kristo yuko hukumuni. Utamtendaje Yesu aitwaye Kristo?

Na matata;
Palipo na giza,
Utaniongoza,
Hivi nitaweza
Kufuata.

Sasa tukiinamisha mioyo yetu kwake. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Yesu Kwa Imani*—Mh.]

227 Wazeni kindani, marafiki. Huenda ikawa jina lako ndilo la mwisho kuandikwa kwenye kile Kitabu. Tuko katika wakati wa mwisho. Sasa wazeni kindani kabisa. Je, kuna mtu hapa ambaye amemkataa?

228 Kumbukeni, huenda isije tena. Pilato hakuwa na nafasi nyingine. Yeye alijaribu alivyoweza kuokolewa, wala asingeweza kufanya jambo hilo. Lilikuwa mikononi mwake. Basi utalitendaje Neno lililotiwa mafuta kwa ajili ya siku hii, liitwalo Kristo?

*Nimtendeje Yesu Aitwaye Kristo?* SWA63-1124M
(What Shall I Do With Jesus Called Christ?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, 24 Novemba, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1994 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org